# Nipashe

Ijumaa Oktoba 2, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMI

ISSN 0856 • Na. 0580356

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




**IGP** Sirro amtaka Lissu ajisalimishe kituo cha polisi

UKURASA 3



**MAREKANI** yasisitiza kutoegemea upande uchaguzi wa Tanzania

UKURASA 4

Mikoa 6 vinara kwa udumavu hadharani

UKURASA 4

**MAMIA** wakacha matibabu ya saratani, wakimbilia kwa sangoma na maombezi... *Endelea ukurasa wa 2*

# HATARI



Mgombea urais wa CCM, Dk. John Magufuli akicheza muziki wa msanii maarufu wa nyimbo za injili, Rose Mhando, katika mkutano wa hadhara wa kampeni mjini Vwawa, wilayani Mbozi, mkoa wa Songwe jana. **PICHA: IKULU**

## JPM: Tutawalinda wazee na kuwathamini

UKURASA 2

**Ardhi yaipiku Polisi baa la rushwa**

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA YAFUATA TATU ZA JKT NA UBINGWA UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6

## HABARI KITAIFA




Katibu Mkuu wa Baraza la Wazee la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Rodrick Lutembeka, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu maadhimisho ya Siku ya Wazee Dunia. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wengi wakwepa tiba rasmi kansa

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Saratani Ocean Road (ORCI), imesema maboresho makubwa yanayoendelea katika huduma zake, yanakwazwa na tatizo kubwa la wagonjwa kukatisha tiba na kuhamia mbadala wa waganga wa kienyeji na nyumba za ibada.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi hiyo, Dk. Julius Mwaiselage, amelalamika kuwa mwenendo huo unaowahusisha wastani wa wagonjwa 500 hadi 600 kutoka idadi ya wagonjwa 7,000 wanaofika kupata huduma za saratani kwa mwaka.

Ametaja sababu kuu ni kurubuniwa na matangazo mbalimbali yasiyo rasmi kuhusu dawa na maudhui yaliyomo katika mitandao ya kijamii.

Dk. Mwaiselage alitoa ufafanuzi huo jana alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam ikiwa ni sehemu ya kuihamasisha jamii uelewa kuhusu saratani na hususan ya matiti, akisema ukiuaji huo ni mwenendo potofu.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, inakadiriwa kuwa asilimia 10 ya wagonjwa wa saratani, ndiyo wanaokatisha matibabu na kukimbilia tiba za asili na huduma za maombezi.

"Hatujafanya utafiti isipokuwa wanaondoka kwa njia zisizo rasmi kwenda kwenye tiba za asili na maombi ni kama asilimia 10 ya wagonjwa wote.

"Imani potofu zilizozagaa mitandaoni na ndani ya jamii ambako watu wanadanganyana kuwa wanaweza kupona saratani kwa njia ya maombi au dawa za kienyeji, zinawafanya wagonjwa kushindwa kuendelea na matibabu," alisema.

"Anakuwa ametibiwa 'stage' (hatua) ya kwanza na ya pili anaacha na kwenda kwenye maombi na kwa waganga wa kienyeji kwa miezi mitatu, anapakwa dawa sijui ni chokaa, akirudi tena hospitali yupo katika hatua mbaya ya ugonjwa kusambaa zaidi na inakuwa ngumu kumtibu na kupona," alisema.

Alisema hospitali hufanya juhudi za kuwafuatilia kwa kuwapigia simu ili kuulizia sababu za kutoendelea na matibabu na hivyo kueleza sababu hizo na wakati mwingine wanapata taarifa kuwa mgonjwa husika ameshapoteza maisha.

"Kwa sababu wanaandika namba zao za simu, tukikaa miezi sita hatujamwona mgonjwa akirudi kuendelea na matibabu, tunalazimika kumpigia simu ili kujua sababu.

"Iwe ni sehemu za maombi au za tiba mbadala, waendelee nazo lakini hao wanaowapa huduma, wasiwazuie wakaacha dawa zetu na kuja kliniki kufanyiwa uchunguzi wa afya zao," alionya.

Mkurugenzi huo pia aliwataka wagonjwa kuzingatia kanuni na ushauri wa madaktari wakati wa matibabu ili kuondokana na madhara yatokanayo na kutozingatia maelekezo wakati wa matibabu.

Dk. Mwaisalege pia alisema taasisi hiyo ya saratani imeongeza idadi ya wagonjwa inaowatibu baada ya kupata mashine za kisasa na dawa maalumu, akibainisha mabadiliko ya kitakwimu kwamba kabla ya mwaka 2015 walikuwa jumla ya wagonjwa 30,000 wanaowatibu kwa mwaka, lakini maboresho yamewafikisha 55,000.

Akizungumzia elimu ya kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa uchunguzi wa mapema wa saratani ya matiti iliyohusisha wanawake waliopona ugonjwa huo wanaofahamika kama mashujaa, Dk. Mwaiselage aliwataka wanawake nchini kujitokeza kupatiwa matibabu kwa sababu ugonjwa huo unatibika.

Alisema nchini wagonjwa wapya wa saratani 42,000 hupatikana kila mwaka na kati yao asilimia 12 ni wagonjwa wa saratani ya matiti.

Oktoba ya kila mwaka ni mwezi maalum uliochaguliwa kuenzea elimu na kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa uchunguzi wa mapema na njia bora za kuzuia maradhi ya saratani ya matiti.

# JPM: Tutawalinda wazee, kuwathamini

**Na Gwamaka Alipipi,** TUNDUMA

MGOMBEA urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, amesema katika kipindi cha miaka mitano ijayo, serikali itaendelea kuwajali, kuwalinda kwa nguvu zote wazee kwa kuwapatia huduma bora, ikiwamo matibabu bure.

Amesema serikali itahakikisha inazidisha ulinzi kwa wazee, kuwalinda kutoka katika mauaji pamoja na kuwapatia makazi bora.

Alitoa ahadi hiyo jana mjini Tunduma mkoani Songwe, wakati akizungumza na maelfu ya wananchi na wanachama wa CCM, waliojitokeza kumsikiliza katika Uwanja wa Shule ya Sekondari Nyerere, akiomba ridhaa ya kuchaguliwa tena kuwa rais.

"Leo ni siku ya wazee duniani, ninapenda kuwahakikishia wazee nchi kwamba tutawalinda kwa nguvu zote, tutaendelea kuwalinda kutoka katika mauaji ya vikongwe, wazee bado hawajapitwa na wakati tunawahitaji, hata mama yangu mimi ni mzee na yupo kitandani hajiwezi," alisema Dk. Magufuli.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano serikali iliendelea kutekeleza sera ya Taifa ya wazee na kupatikana mafaniko lukuki ikiwamo, kuongezeka kwa idadi ya wazee waliopatiwa vitambulisho vya kuwawezesha kupata matibabu bila malipo, kutoka 213,025 mwaka 2015 hadi wazee 1,042,403 mwaka huu.

Alisema wazee wasiojiweza 2,135 wanaishi katika makazi 16 yanayomilikiwa na serikali na kuendelea kupatiwa huduma za msingi za chakula, malazi, mavazi na matibabu.

"Katika kipindi cha miaka mitano tumeboresha makazi ya wazee kwa kukarabati ikiwamo Korandoto, Mabuga-Manyara, Fungafunga-Mara pamoja na Kigamboni Dar es Salaam. Hivyo tutaendeleza juhudi hizo kwa miaka mitano ijayo," alisema.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano serikali iliimarisha upatikanaji wa huduma za afya kwa wazee kwa kuanzisha madirisha 2.335 ya kutolea huduma za afya kwa wazee katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

Kadhalika, alisema katika kipindi hicho, kumeanzishwa mabaraza ya wazee 8,183.

Aliongeza: "Tumedhibiti mauji ya wazee na hasa mikoa ya kanda ya ziwa baada ya kuvielekeza vyombo vya ulinzi na usalama, hii ni kuthibitisha kwamba tutaendelea kuwa na wazee, wazee hawajapitwa na wakati."

Alisema licha ya kuwapo kwa changamoto zinazowakabili wazee nchini, lakini serikali itaendelea kuzitatua na kuwajali.`

# ...Afuta kampeni Mama Komandoo

**Na Gwamaka Alipipi,** TUNDUMA

RAIS John Magufuli amepiga marufuku kampeni ya Mama Komandoo mkoani Songwe, inayowatoza wajawazito Sh. 50,000 pindi wanapochelewa kuhudhuria kliniki.

Sambamba na hilo, amewataka wanawake katika mkoa huo kuendelea kubeba mimba ili kuongeza idadi ya Watanzania.

Alitoa hauli hiyo jana mkoani Songwe, wakati akiomba ridhaa ya kuchaguliwa tena kuwa rais kwa miaka mitano ijayo, pamoja na mambo mengine ametumia nafasi hiyo kupiga marufuku hatua ya wahudumu wa vituo vya afya kuwatoza wajawazito kiasi hicho cha fedha.

"Kuna malalamiko ya Mama Komandoo kuwatoza wajawazito ambao wanachelewa kwenda kliniki. Kwa hiyo mama ukichelewa kwenda kliniki unatozwa Sh.50,000, naifuta leo, kwa hiyo mama komandoo aende kulima mahindi, aachane na tabia ya kutoza akina mama," alisema Dk. Magufuli na kuongeza:

"Mwanamke akipata mimba anawaza kulipa Sh.50,000 wakati hiyo mimba hakuweka mama komandoo yeye anasubiri kutoza fedha tu, sasa natangaza kuanzia leo ni marufuku mjamzito kutozwa pesa, alisema Dk. Dk.Magufuli.

Rais Magufuli alimtaka Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Songwe pamoja na viongozi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kutekeleza agizo hilo mara moja.

Alisema: " Wahusika nadhani mmenisikia, kampeni Mama komandoo ni marufuku kuanzia leo. Akina Mama bebeni mimba vizuri ili tuongeze uchumi , nchi yenye watu wengi ndiyo inaongoza kwa uchumi, China na India ndiyo wanaongoza kwa uchumi kutokana na idadi ya watu walikuwa nao," alisema Rais Magufuli.

Hata hivyo, aliwataka wanawake ambao watapata ujauzito kuhudhuria kliniki ili Taifa liweze kupunguza idadi ya vifo vya Mama na mtoto wakati wa kujifungua.

**KUENDELEZA KILIMO**

Rais Magufuli aliwahakikishia wananchi wa mkoa wa Songwe kwamba serikali itaendeleza kilimo mkoani humo. Alisema mkoa wa Songwe ni mojawapo ya mikoa inayotegemewa katika uzalishaji wa chakula nchini, hivyo serikali lazima iuendeleze.

**ASISITIZA AMANI**

Kadhalika, Rais Magufuli aliwataka Watanzania kuendelea kuitunza amani na kueleza kuwa bila ya amani hakuna anayeweza kufanya shughuli yoyote ya kimaendeleo.

"Hata shamba huwezi kwenda, bila amani huwezi kufungua duka, amani ikipotea umepoteza vyote, bila amani huwezi kwenda hata Msikitini wala Kanisani. Nawaomba Songwe tuitunze amani yetu, Baba wa Taifa enzi za uhai wake hakutaka tumwage damu, tulipata uhuru wetu bila kumwaga, kulikuwa na dini na kabila mbalimbali lakini alisimamia vema,"alisema Rais Magufuli.




Wanawake waliopona na wanaoendelea kupatiwa matibabu ya saratani ya matiti maarufu kama Mashujaa, wakiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Dk. Julius Mwaiselage (mwenye suti nyeusi), wakirusha maputo juu, jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni ishara ya kuadhimisha mwezi Oktoba wa kuhamasisha jamii kuhusu uelewa wa saratani hiyo. **PICHA: MARY GEOFREY**

# Sirro amtaka Lissu ajisalimishe polisi

**Na Joseph Mwendapole**

MKUU wa Jeshi la Polisi (IGP) Simon Sirro, amemtaka mgombea urais wa CHADEMA, Tundu Lissu, ajisalimishe kituo cha polisi mkoani Kilimanjaro.

Akizungumza jana, IGP Sirro alisema jeshi hilo limeshindwa kuvumilia vitendo vya utovu wa nidhamu vinavyofanywa na mgombea huyo wa urais na wanachama wa chama chake.

Alisema Lissu na wenzake wamekuwa wakiwakaripia na kuwagombeza askari wake wanaokwenda kuimarisha ulinzi kwenye mikutano yake ya kampeni inayoendelea.

"Jana niliongea na kiongozi wake Mbowe ili awaambie watu wake na Lissu kwamba anayoyafanya Watanzania wenye hekima na wazalendo wa nchi hii wanayaona, Lissu ajue hayuko juu ya sheria, polisi tukiamua kuchukua hatua asilalamike, yeye hana uwezo wowote wa kupambana na Jeshi la Polisi," alisema.

"Nasema aende akaripoti kituo cha polisi Kilimanjaro akaeleze aliyoyafanya jana kwa sababu wanasiasa lazima watambue kuwa bila amani na utulivu hawawezi kuendesha siasa," alisema IGP Sirro.

Alisema vyama vya siasa vinavyopambana kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka huu viko 12 na Jeshi la Polisi limepewa wajibu wa kusimamia sheria kuhakikisha kampeni zote zinafanyika kwa amani.

"Sasa yeye asifikiri kwamba anauweza wa kupambana na polisi, niwaombe sana wanachama wa CHADEMA waache na nitoe wito kwa wanachama wote wa vyama vya siasa tuheshimu sheria za nchi," alisema Sirro.

Alisema inaonekana kuna baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa ambao wanataka kusababisha vurugu ili uchaguzi wa mwaka huu uahirishwe jambo ambalo alisema halipo. "Uchaguzi mkuu lazima utafanyika, lakini wale ambao wanataka kusababisha fujo itafika wakati tutawashughulikia," alisema Sirro.

# TAKUKURU yataja ardhi kuongoza rushwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU) mkoani Dodoma, imeitaja sekta ya ardhi kuongoza kwa malalamiko ya vitendo vya rushwa kwa asilimia 60.

Akitoa taarifa jana ya utekelezaji wa majukumu ya taasisi hiyo kwa mwezi Julai hadi Septemba 2020, Mkuu wa TAKUKURU Dodoma, Sonsthenes Kibwengo, alisema wamepokea taarifa 482 za rushwa na inaonyesha sekta hiyo kuongoza ikifuatiwa na vyama vya siasa kwa asilimia 12.

Alisema kwa upande wa sekta ya ujenzi ni asilimia tano, mikopo umiza, asilimia tano na polisi ni asilimia nne.

Kadhalika, alisema wamekamilisha uchunguzi wa majalada 16 na kufungua mashauri 15 mahakamani, sita yametolewa uamuzi na mahakama na Jamhuri imeshinda mashauri manne.

Katika hatua nyingine, Mkuu huyo alisema taasisi hiyo imeokoa Sh. bilioni 1.27 ambazo zilipaswa kurejeshwa serikalini, vyama vya ushirika na wananchi.

Kati ya fedha hizo Sh. milioni 323.6 waliipwa na kandarasi kinyume cha mikataba au bila kufanya kazi, fedha zilizokusanywa bila kuwasilishwa sehemu husika, malipo batili kwa watumishi na madeni sugu ya viongozi na wanachama wa vyama vya akiba na mikopo.

"Kati ya fedha hizo Sh. milioni 81.6 zimerejeshwa na makandarasi na watumishi wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), waliolipwa bila kustahili, hii inafanya jumla ya fedha zilizorejeshwa TARURA kuanzia Juni 2020, kufikia Sh. milioni 104.4 kati ya Sh. milioni 124.5," alisema.

# ACT- yataka ofisa wao afikishwe mahakamani

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimelitaka Jeshi la Polisi nchini, kumfikisha mahakamani Ofisa Habari Msaidizi wa chama hicho, Dotto Rangimoto, ambaye anasota kituo cha polisi kwa takribani wiki moja.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Ngome ya Vijana ya chama hicho, Abdul Nondo, alisema mtuhumiwa huyo ana haki zake, ambazo hadi sasa zimevunjwa.

Alisema Rangimoto anatuhumiwa kwa makosa ya mtandaoni na kwamba kisheria hairuhusiwi kumweka rumande mtuhumiwa kwa zaidi ya saa 48, bila kumpeleka mahakamani.

Akielezea kukamatwa kwa ofisa huyo, alisema alikamatwa akiwa ofisini na kumkamata yeye na maofisa wengine.

"Wawili walipewa dhamana siku mbili baadaye katika Kituo cha Polisi Osterbay na yeye kubaki chini ya kizuizi cha Jeshi la Polisi kituoni hapo," alisema.

Aidha, Nondo alisema hadi sasa hakuna ndugu, jamaa na mwanasheria wake aliyeruhusiwa kumwona, jambo ambalo si sawa kwa mujibu wa sheria.

Rangimoto na maofisa wengine wawili walikamatwa Ijumaa iliyopita na Jeshi la Polisi lilithibitisha kuwashikilia watu hao na baadaye wawili waliachiwa kwa dhamana.

**Imeandikwa na Frank Maxmilian na Evelyneneema Ernest**

HeliumOne

TATHMINI YA ATHARI ZA MAZINGIRA NA JAMII

TAARIFA YA AWALI YA MRADI TARAJIWA WA UTAFUTAJI GESI YA HELIUM KWA NJIA YA UCHORONGAJI KATIKA WILAYA YA MOMBA, MKOA WA SONGWE-

2159925902

Kampuni za Gogota (Tz) Limited na Njozi (Tz) Limited zinamiliki leseni za utafutaji wa madini katika vitalu vyenye jumla ya kilomita za mraba 4,192.7 katika eneo la mashariki mwa bonde la Rukwa, kusini mwa Tanzania. Kampuni hizi zinataka kujiridhisha kuhusu uwepo wa gesi ya Helium. Gesi hiyo inatarajiwa kuwa na kiwango cha kati ya asilimia 4.2 na 10. Kabla ya mradi wa uzalishaji gesi kutekelezwa tafiti mbalimbali zimepangwa kufanyika na kati ya tafiti hizo ni tafiti kwa njia ya uchorongaji. Jumla ya visima vinne vinatarajiwa kuchorongwa katika maeneo mbalimbali ya mradi. Baada ya kumalizika kwa utafiti, visima hivi vitafunikwa mpaka pale uzalishaji utakapoanza.

Utafiti huu unatarajiwa kufanyika katika Kata za Kamsamba, Ivuna, na Mpapa katika Wilaya ya Momba, Mkoa wa Songwe. Uchorongaji unatarajiwa kuanza mwezi wa pili 2021 na unatarajwa kumalizika ndani ya miezi minne. Kwa mantiki hiyo kampuni za Gogota (Tz) Limited na Njozi (TZ) chini ya kampuni ya Helium One zimepanga kufanya tafiti hizi za athari zinazoweza kutokana na uwepo wa mradi huu kwenye mazingira na kijamii. Hivyo basi maombi ya kufanya tathmini hii yamefanywa kwa pamoja kati ya kampuni hizi mbili za Gogota (TZ) Limited na Njozi (TZ) Limited, hivyo cheti cha mazigira kitatolewa kwa Gogota (TZ) Limited na Njozi (TZ) Limited.

Kwa mujibu wa sheria za usimamizi wa mazingira kipengele namba 20 ya mwaka 2004, na sheria nyenza ya udhibiti na ukaguzi wa mazingira ya mwaka 2005, na marekebisho yake ya mwaka 2018, taarifa hii inawasilishwa kuufahamisha umma kwamba kampuni ya MTL Consulting Limited imepewa kazi ya kufanya tathimini ya athari za mradi huu wa uchorongaji wa visima kwenye mazingira na jamii kwa niaba ya kampuni za Gogota (Tz) Limited na Njozi (TZ). Tathmini hii itafanyika katika kata tatu zitakazojumuisha vijiji vya Kamsamba, Mkonko, Usoche, Mpapa, Masanyita, Kasanu, Lwatwe, Samang'ombe na Itumbula.

Taarifa hii inachapishwa ili kukusanya maoni, maswali, na ushauri kutoka kwa wadau wote wa mradi. Mdau yeyote mwenye maoni au taarifa yoyote juu ya athari zinazoweza kusababishwa na mradi huu kwenye jamii na mazingira awasiliane au atume maoni yake kwenye ofisi zifuatazo:

| | | |
|---|---|---|
| Mkurugenzi<br>Gogota (Tz) Limited and Njozi (Tz) Limited.<br>Gorofa ya Pili, Kilwa House, 369 Toure Drive, Oyster Bay<br>S.L.P 62, Dar Es Salaam,Tanzania<br>Mawasiliano+255 22 2600594 | Mkurugenzi Mkuu<br>Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC)<br>Ofisi ya Kanda ya Magharibi,<br>NSSF MAFAO House, Gorofa ya Kwanza<br>S.L.P 974, Kigoma/Ujiji, Tanzania.<br>Mawasiliano:+255-788825359<br>Barua pepel:.nemckigoma@nemc.or.tz | Meneja Mkuu<br>MTL Consulting Company Limited<br>Masaki, Nyumba namba 2,Kitalu 689<br>Barabara ya Sandvik<br>S.L.P 77894<br>Dar es Salaam, tANZANIA<br>Simu ya Mezani: *+255 22 2600594,*<br>*Simu ya mkononi: +255 767 360 225*<br>Barua pepe:info@mtlconsulting-tz.com |

# Marekani: Hatumuungi mkono mgombea yeyote

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Marekani imesema haimuungi mkono mgombea yeyote au chama chochote katika uchaguzi wa Tanzania, bali inaunga mkono mchakato wa kidemokrasia pekee.

Kwa mujibu wa tamko lililotolewa jana na serikali hiyo kupitia Ubalozi wa Marekani nchini, inaunga mkono mchakato wa kweli wa uchaguzi ulio huru, wa haki na wenye uwazi kabla, wakati na baada ya siku ya uchaguzi.

Taarifa hiyo ilifafanua kuwa mchakato huo unapaswa kuwa na usalama wa wagombea wote, kuheshimiwa kwa utawala wa sheria, na hali ya mamlaka na vyombo vilivyopewa wajibu wa kusimamia na kuendesha uchaguzi kwa kutopendelea upande wowote.

"Marekani, pamoja na nchi nyingine za kidemokrasia, itafuatilia kwa karibu matendo ya watu wanaoingilia na kuvuruga mchakato wa kidemokrasia au kuchochea vurugu dhidi ya raia kabla, wakati au baada ya uchaguzi," ilifafanua tamko hilo. "Hatutasita kufikiria kuchukua hatua stahiki kwa wale watakaobainika kuhusika katika vurugu na machafuko yanayohusiana na uchaguzi au kukwaza mchakato wa kidemokrasia," alisema.

Tamko hilo lilifafanua kuwa, Marekani inaunga mkono wito uliotolewa na wagombea wakuu wa kuwapo kwa mchakato wa uchaguzi wa amani na wenye uwazi na tunatoa wito kwao na kwa wafuasi wao kuchukua hatua kutanzua hali ya uhasama inayojengeka na kuepuka matamshi ya kichochezi.

Tamko hilo lilieleza kuwa, uendeshaji wa uchaguzi mwingine nchini utakuwa na matokeo muhimu si kwa Tanzania yenyewe pekee, bali pia kwa kanda nzima ya Afrika Mashariki.

"Historia ya Tanzania ya kuendesha chaguzi zinazohusisha vyama vingi inarudi nyuma hadi miaka 25 iliyopita na kuifanya nchi hii kuwa mfano wa kuigwa katika bara hili," lilisema tamko hilo.



Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la Heatlh Promotion Tanzania (HDT), Dk. Peter Bujari, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, akiwataka wahisani kuisamehe madeni Tanzania ili fedha zitakazopatikana zitumike kuimarisha miundombinu ya sekta ya afya. Kushoto ni Ofisa Mhamasishaji wa Shirika hilo, Norah Kimwaga. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Shirika lataka Tanzania ifutiwe madeni

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la huduma za afya la Health Promotion Tanzania (HDT), limeomba wahisani kuisamehe madeni Tanzania ili fedha zitakazopatikana zitumike kuimarisha miundombinu ya sekta ya afya.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa HDT, Peter Bujari, alisema shirika hilo kwa sasa linafanya kampeni ya wiki moja kuhamasisha nchi na mashirika yaliyoikopesha Tanzania, isamehe mikopo au ruzuku.

"Tunaomba ama yasamehe au kuahirisha kudai ili fedha ambazo zingetakiwa kulipwa zitumike kuimarisha miundombinu ya afya kwa ajili ya kujiandaa na milipuko ya magonjwa baadaye," alisema.

Alisema mwaka 2012/13 serikali kupitia vyanzo vyake vya ndani ilitegemea kukusanya Sh. trilioni 13.6 kutoka vyanzo vyake na imeongezeka hadi Sh. trilioni 23 mwaka huu wa fedha. Alisema mwaka 2012/13 katika bajeti ya serikali ilikopa Sh. trilioni 5.01 kutoka maeneo mbalimbali duniani na mwaka 2020/21 mikopo ilikuwa ni Sh. trilioni 10.6.

Bujari alisema kwa mujibu ya utafiti uliofanywa mwezi Juni na Shirika la Fedha Duniani (IMF) mwezi, inakadiria kwamba ukuaji wa uchumi kwa Tanzania utashuka kutoka 6.9 mpaka 2.5.

"Moja ya sababu ni vyanzo vyetu vya mapato yatokanayo na utalii ambao baada ya nchi kufunga mipaka yake kwa sababu ya corona, watalii walikuwa hawaji, kwa makisio ni kwamba mapato yanapungua," alisema.

Alisema licha ya changamoto hizo bado wanaodai wanataka walipwe madeni yao ambayo yalikopwa zamani.

"Ikiwa tutawalipa kama tulivyokusudia maana yake hatutakuwa na fedha za kujiendesha na kama mnakumbuka corona ilileta changamoto hatukuwa na miundombinu ya kuwezesha kukabiliana nao," alisema.

Alisema wadau wa afya wanaona ni wakati wa kujipanga kama nchi kuboresha miundombinu ya afya ili itakapotokea janga lingine, mifumo iweze kuwasaidia Watanzania.

Alisema mwaka wa fedha 2020/21 bajeti ya serikali iliyopitishwa bungeni ni Sh. trilioni 34.878 na imepanga kulipa madeni ya Sh. trilioni 10.4 sawa na asilimia 29.9.

Bujari alisema mapato ya ndani yanayokusanywa ni trilioni 24.07 sawa na asilimia 69 ya bajeti.

Bujari alisema ni wakati wa wakopeshaji wafikirie namna ya kuzisaidia nchi walizozikopesha badala ya kuongeza madeni mengine.

Alisema Juni mwaka huu, IMF walipitisha uwezekano wa kuipa Tanzania dola za Marekani bilioni 14.3 na Benki ya Dunia (WB) kuna uwezekano wa kutoa dola za Marekani milioni 3.98.

"Tumeiandikia barua leo (jana) Benki ya Dunia kuomba watakapoanza mkutano wao wiki ijayo nchini Marekani ujumbe huu uwe umewafikia watekeleze utoaji wa fedha hizi,"alisema.

Alitaja wengine ambao wanaikopesha Tanzania na kiwango cha fedha kwenye mabado ni Benki ya Exim ya Korea Kusini (dola 501,169), DABEA (dola milioni 1.7), Umoja wa Ulaya (Euro milioni 27).

Aprili, Rais John Magufuli aliiomba Benki ya Dunia badala ya kukopesha nchi zilizokumbwa na corona isamehe madeni waliyokopesha.

# Mikoa vinara kwa udumavu yaanikwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Kilimo imetaja mikoa sita ambayo inaongoza kwa kuzalisha chakula kwa wingi, huku ikikabiliwa na tatizo la udumavu kwa watoto.

Kufuatia hali hiyo, imeandaa mpango mkakati wa kitaifa wa masuala ya lishe ili kuondoa tatizo hilo nchini.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini Dodoma, Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, alitaja mikoa hiyo ni Njombe, Iringa, Kigoma, Ruvuma, Rukwa na Songwe.

Mgumba alisema mikoa hiyo inazalisha chakula kwa viwango vikubwa, lakini ndio inaongoza kwa kuwa na udumavu.

Alisema serikali imejipanga kutokomeza tatizo hilo kwa kutoa elimu juu ya matumizi ya vyakula vya kuongeza lishe.

"Serikali imejipanga kuhakikisha mikoa hiyo inaondokana na udumavu, hivyo kupitia siku ya chakula duniani, wataalamu watatoa elimu jinsi ya matumizi ya vyakula vya lishe, " alisema Mgumba.

Naibu waziri huyo alisema Mkoa wa Njombe una udumavu kwa asilimia 53.6, huku ukizalisha chakula tani 446,491.

Alibainisha Mkoa wa Rukwa una asilimia 47.9 ya udumavu wakati inazalisha chakula tani 943,002, huku kiwango cha utoshelevu ni asilimia 230.

"Mkoa wa Iringa una asilimia 47.1 ya udumavu wakati unazalisha tani za chakula 470,750 kiwango cha utoshelevu ni asilimia 161, Songwe ina asilimia 43.3 wakati unazalisha chakula tani 805,545 kiwango cha utoshelezi ni asilimia 210," alisema.

Alisema Mkoa wa Kigoma una asilimia 42.3 ya udumavu, huku ukizalisha tani 1,158,214 kiwango cha utoshelezi 165 na Ruvuma una asilimia 41.0 ya udumavu na unazalisha tani 1,251,511 kiwango cha utoshelezi ni 237.

Alisema mpango huo unaanza mwaka 2020/21 ikiwa ni sehemu ya programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) ambao unaainisha majukumu mbalimbali ya wadau katika kuchangia kupunguza lishe duni nchini.

Aidha, alisema wizara inaendelea kuboresha miongozo mbalimbali na kutoa elimu namna ya kuzalisha kuhifadhi na kutumia mazao ya mikunde kama vile soya, choroko, mbaazi na dengu ambayo yana viini lishe aina ya protini.

Katika hatua nyingine, Mgumba alisema wiki ya chakula itazinduliwa Oktoba 10, mwaka huu ambalo litakuwa na dhumuni la kuwawezesha wakulima, wafugaji na wavuvi kujifunza teknolojia sahihi za kuongeza uzalishaji na mbinu za kutokomeza njaa.

HABARI KITAIFA

# Mbaroni madai kukutwa na meno ya tembo, silaha

**Na Julieth Mkireri,**
KIBAHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani linawashikilia watu wanane kwa tuhuma za kukutwa na meno ya tembo kilogramu 2 yenye thamani ya Sh. milioni 52 na silaha sita aina ya gobore.

Watuhumiwa hao ni kati ya 95, waliokamatwa katika operesheni iliyofanywa na jeshi hilo kuanzia Septemba mosi hadi 30, mwaka huu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema meno hayo ya tembo yalikamatwa Chalinze kwenye nyumba za watuhumiwa hao, ambao wanadaiwa kuwa wawindaji haramu.

Wankyo alisema katika operesheni hiyo watuhumiwa 64 tayari wamefikishwa mahakamani, wakiwamo waliokamatwa na meno ya tembo.

Alisema pikipiki 20 pia zilikamatwa pamoja na watuhumiwa 11, mali nyingine zilizokamatwa ni kompyuta mpakato, deki mbili, mitungi ya gesi, jenereta moja, redio na luninga moja.

"Operesheni hii ilifanyika pia katika bandari bubu, ili kudhibiti wafanyabiashara wanaotumia bandari hizo kupitisha bidhaa isiyolipiwa ushuru, ambapo watuhumiwa sita walikamatwa na kuokoa mafuta ya kula lita 3440 na diseli lita 240," alisema.

Aidha, alisema watuhumiwa 41 wa dawa za kulevya za viwandani na mashambani zilikamatwa, ambapo kilogramu 120.7 za bhangi, mirungi bunda 42 na dawa aina ya heroin kilogramu 500.

Kamanda Wankyo alisema, wasafirishaji wa dawa hizo wameanza kutumia mbinu ya kusafirisha kwa kutanguliza pumba na kuweka dawa ndani pamoja na matenga ya nyanya.



Wawakilishi wa umoja wa wanafunzi waliohitimu Shule ya Sekondari Keko miaka tofauti (KEKO ALUMNI), wakizungumza na wanafunzi wa kidato cha nne, ili kuwatia moyo, kuwapa motisha na kubadilishana nao mawazo juu ya masuala mbalimbali ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya kuelekea mitihani yao ya mwisho ya kuhitimu, walipotembelea shuleni hapo, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mali Ngurdoto kupigwa mnada kulipa malimbikizo mishahara

**Na Woinde Shizza,**
ARUSHA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Arusha, Masijala Ndogo ya Kazi, imetoa hati ya kukamata kwa mitambo miwili mikubwa ya kufua umeme (jenereta), mali ya Hoteli ya kitalii ya Ngurdoto.

Uamuzi huo umefikiwa baada ya mahakama hiyo kusikiliza shauri la madai, namba 98 la mwaka 2018.

Jana, Msajili wa Mahakama hiyo, John Mkwabi, aliiambia mahakama kuwa ameridhia kukamatwa kwa mali hizo, ili kufidia deni linalotokana na malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi.

Kwa mujibu wa Msajili, mahakama hiyo ilipokea maombi ya upande wa mashtaka na kutoa hati ya kukamatwa kwa jenereta hizo, ili kufidia malipo ya Sh. 231,000,000 yanayotokana na malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi.

Awali, Ofisa kazi Mkoa wa Arusha, Emmanuel Mweta, alisema kuwa awali mali zilizokuwa zimeombwa kukamatwa ni magari mawili, ambayo yamebainika kutokuwapo kwenye kumbukumbu ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kama mali za mdaiwa.

"Mheshimiwa Msajili tunaiomba mahakama kubadilisha mali za kukamatwa baada ya magari mawili tuliyokuwa tumeomba kutokuwamo kwenye kumbukumbu ya TRA na hivyo tunapendekeza mali nyingine, ambayo ni jenereta mbili aina ya katapila lenye ukubwa wa umeme wa msongo wa kilovolti (KV 400), ambayo ni mali ya mdaiwa," alisema Mweta.

Pia, Mweta alitoa maombi ya kupata hati ya kuvunja sehemu ya jengo la hoteli hiyo iliyokuwa imejengewa jenereta hiyo, ili liweze kutolewa.

Hata hivyo, Msajili Mkwabi aligoma kutoa hati mara mbili na kutoa maelezo ya kuendelea na zoezi hilo na kama kutakuwa na tatizo mdaiwa atapaswa kufika mahakamani.

Shauri hilo limeahirishwa hadi litakapotajwa tena Oktoba 27, mwaka huu. Hata hivyo, Msajili aliagiza utekelezaji wa ukamataji wa jenereta hizo uwe umekamilika ifikapo Oktoba 20, mwaka huu.

Wakati huo huo, mahakama hiyo imeamuru kuuzwa kwa mali za mdaiwa, ambaye ni hoteli ya Naura Spring zinazoshikiliwa na dalali wa mahakama na zoezi hilo liwe limekamilika Novemba 17, mwaka huu.

Mahakama hiyo imetoa oda ya kukamatwa kwa jenereta na gari moja aina ya Noah, mali ya mdaiwa, ili kufidia deni la Sh. 32,000,000, linalotokana na malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi.

Maombi ya kukamata mali hizo yametolewa mahakamani hapo na Ofisa Kazi, Emmanuel Mweta, ambaye aliiambia mahakama katika shauri la madai namba 83/2019, kwamba mali zilizokuwa zimeombwa hapo awali zina thamani kubwa na hivyo kuiomba mahakama hiyo kukamata mali zingine.

Pia, Mweta aliiomba mahakama hiyo kumpangia tarehe ya mnada wa kuuza magari matatu yanayoshikiliwa na dalali wa mahakama.

Wakili anayemwakilisha mdaiwa, Herode Biliamutwa, alidai hana pingamizi na maombi hayo, na Msajili wa mahakama hiyo, John Mkwabi, aliamuru ifikapo Novemba 12, mwaka huu, mali zilizokuwa zimepatikana ziwe zimeuzwa.

Shauri hilo limeahirishwa hadi Novemba 2020, mwaka huu, litakapotajwa tena.

## JKCI: Takwimu shinikizo la damu zinatisha

**Na Joseph Mwendapole**

SHINIKIZO la damu ni tatizo linaloongoza kwa idadi kubwa ya wagonjwa wanaofika kwenye Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), takwimu zinaonyesha asilimia 70 wanakabiliwa na tatizo hilo.

Hayo yalisemwa jana na Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Moyo wa JKCI, Samweli Rweyemamu, alipofanya mahojiano na waandishi wa habari katika Viwanja vya Tanganyika Packers.

Alikuwa akizungumza wakati wa maadhimisho ya Siku ya Moyo Duniani, ambayo hufanyika Septemba 29, kila mwaka. Dk. Rweyemamu alisema wapo pia wagonjwa wengine wanaokabiliwa na tatizo la kuziba kwa mishipa ya damu inayosambaza damu kwenye moyo ambayo husababisha kifua kuuma.

"Kuna wengine wanaohitaji upasuaji tunaona idadi inaongezeka kila siku, kwa mfano wale ambao mishipa ya damu inaziba tunawazibua kwa upasuaji mkubwa (open heart surgery) au ule mdogo kwa kutumia mtambo wa Cathlab. "Tunaona wagonjwa wanaofanyiwa upasuaji wanaongezeka, mwaka jana hadi Desemba, kwa kutumia mtambo wa Cathlab, tuliwachunguza na kuwatibu wagonjwa 1,409 hii ni idadi kubwa, wagonjwa hawa hapo kabla tulikuwa tunawapa rufani kwenda nje ya nchi," alisema.

Dk. Rweyemamu alitoa mfano kuwa hivi karibuni katika Wilaya ya Temeke, Viwanja vya Zakheem, kupima watu 103, asilimia 18 walikuwa na shinikizo la damu, wengine moyo umetanuka, kati yao wagonjwa 21 walionekana wana matatizo ya moyo.

"Tulienda pia Viwanja vya Mwembe Yanga na kupima watu 150, asilimia 22 walionekana wana magonjwa ya moyo kati yao asilimia 19 walikuwa na shinikizo la damu la juu ," alisema.

"Utaona ni idadi ndogo tunapima, lakini utafiti uliofanyika Dar es Salaam, zinaonyesha karibu asilimia 30 wana shida ya shinikizo la damu, sasa ukiwa na shinikizo la damu ni 'risk factor' ya kuziba kwa mishipa ya moyo hatimaye utafika (JKCI), tukuzibue kwa vifaa maalum," alisema.

Dk. Rweyemamu alisema mtu akiwa na shinikizo la damu moyo hutanuka na kuwa na dalili za moyo kushindwa kufanya kazi kwa hiyo asilimia kubwa ya matatizo ya moyo kwa watu wazima yanaanza na shinikizo la damu.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Prof. Mohamed Janabi, alisema magonjwa ya moyo huchangia karibu asilimia 31 ya vifo vyote duniani na kwamba takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), zinaeleza kila mwaka takriban watu milioni 18 hufariki dunia kwa magonjwa hayo.

"Ni tatizo linaloonekana kuongezeka, takwimu zinaonyesha katika kila mwanamke mmoja kati ya wanne na mwanaume mmoja kati ya watano wanakabiliwa na tatizo la shinikizo la damu," alibainisha.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wazee wanayo mahitaji mengi, watimiziwe sasa

**OKTOBA** mosi ya kila mwaka yaidhinishwa kuwa ni Siku ya Wazee Duniani, lakini huadhimishwa ulimwenguni kwa namna tofauti.

Inafahamika kuwa wazee ni hazina kwa maendeleo ya taifa, kwenye nyanja mbalimbali. Wazee waliokuwa na utaalamu, hutumiwa ama kutegemewa katika kutoa ushauri wao kwa jamii inayowazunguka. Tanzania pamoja na kuungana na nchi nyingine ulimwenguni katika kuidhimisha nchini kuna mambo, ambayo tunatakiwa kuyatekeleza tukizingatia ule msemo wa wahenga "kitunze kidumu" hatunabudi kuwahudumia wazee ipasavyo katika ngazi zote kuanzia familia, jamii na kitaifa kwa ujumla wake.

Kwa mujibu wa taarifa zilizowekwa kwenye mtandao wa Umoja wa Mataifa (UN) ulimwengu unaadhimisha miaka 30 ya Siku ya Wazee Duniani inapotathmini athari kali na mbaya zilizosababishwa na janga la COVID-19, kwa wazee ulimwenguni kote.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, kupitia ujumbe wake alioutoa jana, kuhusu siku ya jana ya wazee duniani ni kwamba Covid-19 imewaathiri wazee sio tu kwa afya zao, bali hata kuhusu haki zao na ustawi wao.

Guterres alikaririwa akibainisha kuwa, wakati ulimwengu unapotafuta kupona vizuri kwa pamoja, lazima wanadamu wafanye juhudi za pamoja katika kipindi cha miaka kumi kilichopewa jina muongo mmoja wa kuzeeka kwa afya yaani mwaka 2020 hadi 2030 kuboresha maisha ya wazee, familia zao na jamii.

Taarifa za UN (1999) zilionyesha kuna ongezeko la idadi ya wazee duniani, ilionekana zaidi katika nchi zinazoendelea, ambapo viwango vya ongezeko havilingani na uwezo wa rasilimali zilizopo kuwahudumia katika nyanja za afya, lishe na huduma nyingine za msingi kwa maisha ya binadamu.

Matarajio ya UN ilikuwa ifikapo mwaka 2050, idadi ya wazee, kwa mara ya kwanza katika historia ya binadamu, itaongezeka na kuzidi ile ya watoto/vijana chini ya miaka 24.

Idadi hiyo katika bara la Afrika pekee inategemewa kuongezeka kutoka milioni 38 ya sasa na kufikia milioni 212 ifikapo mwaka 2050. Tanzania iliamua kuangalia hali na mazingira ya wazee nchini, hivyo ikaona umuhimu wa kuwa na Sera ya Taifa ya Wazee 2003, iliyokusudiwa kutumika kama mwongozo katika utoaji huduma na ushiriki wa wazee katika maisha yao.

Sera ya Taifa ya Wazee ililenga mambo kadhaa, ikiwamo kutambua wazee kama rasilimali muhimu katika maendeleo ya taifa, kuwashirikisha wazee katika maamuzi muhimu yanayowahusu wao na taifa kwa ujumla. Kuboresha huduma zao na kuwapa ulinzi wa kisheria kama kundi maalum, kuwaelimisha vijana kuhusu masuala ya uzee na kuzeeka na kuwajengea uwezo wa kufanya maandalizi ya maisha kuelekea uzeeni. Tunajionea wazi kuwa sera hiyo ni nzuri, ingawa kunahitajika ari na kasi katika kuitekeleza, ili kuepuka malalamiko kutoka kwa wazee hasa wanapokwenda kupata huduma za kiafya, ambapo kwa upande wao zinatolewa bure kulingana na utaratibu uliowekwa.

Malalamiko yamekuwa yakizuka kutoka kwa wazee kuhusu huduma za afya, hasa upatikanaji wa dawa, kwamba wanafanikiwa kuwaona madaktari, lakini wanapofika kwenye maduka ya dawa majibu ya kwamba dawa hii haipo ndiyo yamegeuzwa kama wimbo kwa baadhi ya hospitali.


Kwa kuwa uzee hauna mwenyewe bali ni neema ya pekee kutoka kwa mwenyezi Mungu kila mtu anawajibika kutambua kwamba ni mzee wa kesho, hivyo anapaswa kushiriki katika kujenga mazingira mazuri yanayowanufaisha.

Siyo sahihi kuwabeza na kutojiandaa kuukabili uzee kwa kuwekeza na kuwa na matumizi mazuri ya rasilimali zote zilizokuwamo za familia na taifa kwa ujumla, ili tusije kuishia kuilaumu serikali, maana usipojipanga utapangwa. Tunasisitiza kwamba wazee wana mahitaji muhimu, hivyo jambo la msingi ni kuwatimizia mahitaji yao ya msingi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Yasmine Protace

## Muungwana Lazima Nilonge

# Yajue maadili yalivyokuwa siri ya ufanisi masomoni

**MAADILI,** kimsingi yana maana kuwa mafundisho yanayotolewa katika nafasi mbalimbali, hasa katika malezi ili kumuelekeza binadamu atende namna ambayo inamjenga yeye na jamii nzima kwa ujumla.

Kuna maadili ya namna mbalimbali, kulingana na mifumo ya maisha, vilevile mwenendo ambao jamii ambayo inayo. Hapo kuna misingi ya mila, imani, utamaduni na mazingira walio nayo.

Maadili ya jumla kwa jamii yanfanana kwa karibu sana, ingawa katika sura ya pili, yanaweza yakapishana kwa namna fulani, hata kukaonekana utekezaji kuna tofauti kiasi, miongoni mwa wahusika.

Pamoja na hayo, watu tangu zamani wametoa maadili katika namna maalumu kulingana na dini, utamaduni na falsafa za mahali, au makundi ya watu.

Kwa ujumla, maadili yanatakiwa yazingatie kutolewa kwa makundi mbalimbali na yafikie hatua ya kuzaa matunda, sasa au baadaye.

Mjumuiko wa umma unakosa maadili katika sehemu waliko, kuna kila namna ya kuchangia mambo yake yasiende vyema.

Ndani ya mtazamo huo, hivi karibuni Mkurugenzi Mtendaji wa Shule ya Victoria, iliyopo Mkuranga mkoani Pwani, Peter Mutembei, anajisifu kwamba shule yao imewajenga watoto kimaadili, hata ikawa hali inayowasaidia kufanikiwa kitaaluma.

Katika hilo, Mutembei anarejea hata matokeo mitihani ya kidato cha nne na cha pili kufanywa vizuri kila mwaka shuleni hapo, ni zao la maadili yanayopatikana kwa wanafunzi wao, yamekuiwa ya manufaa makubwa kusaidia watoto wa kike kumaliza elimu yao bila ya ujauzito.

"Watoto tumewajenga kimaadili, shule yetu ina miaka zaidi ya 20, hakuna mtoto wa kike aliyeacha shule kwa kupata ujauzito," anasema na kuongeza kwamba kikubwa kinachotakiwa katika hilo ni umakini katika kuangaliwa ni maadili.

Anasema katika uhalisia, inapotokea mtoto anafaulu masomo pasipo kuwa na maadili sahihi anaishia katika kuhangaika, kwa sababu anachopata katika mtazamo wa utaalamu na uadilifu inaishia pabaya, kwani anakuwa na mwenendo unaokinzana na mahitaji yaliyoko, sababu kuu ni maadili.

Mutembei anafafanua kwamba, kuna haja kubwa ya wanafunzi kulelewa ndani ya maadili, ili anapomaliza masomo yake awe wa manufaa kijamii kwa ujumla.

Mkurugenzi huyo sasa anapenda kuweka msisitizo kwa watoto, pale wanahitimu masomo watoto na kurejea mitaani penye makazi yao, wanakutana na makundi ya aina mbalimbali kimaadili na wanakuwa hatarini kujiingiza katika yasiyofaa.

Kwa mujibu wa Mutembei, suala la maadili wamekuwa wakiwasimamia watoto kunazia wanapoingia shuleni na wakionekana kukosa hayo maadili,wanawafunza katika sura ya kuwarekebisha hata wakafuata mstari stahiki wa kimaadili.

Ana maelezo ya siri ya mafaniko katika ufaulu wa shule, unatokana na msingi wa mafunzo ya maadili walionayo na namna ya kufanikisha kumrekebisha mtoto.

Mutembei anaitaja kuwa ndio namna msingi aliyo nayo alikotoka na kama hakuwa na mwanzo mzuri kinidhamu, inamgharimu katika wepesi wa kumrekebisha.

Anasema maadili yanaanzia kwa watoto wakiwa wadogo kwa kuelekezwa nini wanatakiwa kuifanya na kipi hawatakiwi kukifanya na kwa kwa kufanya hivyo kutasaidia mtoto kumjenga kimaadili.

HABARI KITAIFA

# Makamba aahidi ujenzi zahanati 20

**Na Thobias Mwanakatwe**

MBUNGE mteule wa Jimbo la Bumbuli mkoani Tanga kupitia CCM, January Makamba, amesema katika kipindi cha miaka mitano ijayo amejipanga kusimamia ujenzi wa zahanati 20 na vituo vya afya vipya viwili.

Akizungumza katika mikutano ya kampeni anayoendelea kuifanya katika jimbo hilo, alisema lengo la kujenga zahanati na vituo vya afya ni kusogeza huduma za afya karibu na wananchi pamoja na kutekeleza sera ya kuwa na zahanati kila kijiji.

Makamba ambaye amepita bila kupigwa katika jimbo hilo, alisema awali alipoingia madarakani alikuta zahanati nane, lakini hivi sasa zipo mpya 20 zinazoendelea kujengwa katika maeneo yote ya jimbo hilo.

Alisema Oktoba 28, mwaka huu wajitokeze kwa wingi kwenda kumchagua na kumpa kura nyingi mgombea urais wa CCM, Dk. John Magufuli.

Alisema Dk. Magufuli ni mgombea anayetokana na chama chenye sera, ilani bora na mipango inayojibu shida, matakwa na mahitaji ya Watanzania.

Pia, aliwaombea kura wagombea wa ngazi ya udiwani wanaotokana na CCM, kwa kuwa chama hicho kinachuja na kupika viongozi wake.

Aliongeza sababu nyingine ya kuichagua CCM ni kutokana na rekodi na historia ya kutekeleza ahadi zake na kuongoza kwa amani.

# Waliopigana vita vya pili ya dunia kuishtaki Uingereza

**Na Yasmine Ptotace**

WAZEE waliopigana Vita Kuu ya Pili ya Dunia, wameiomba serikaki iwasaidie rasilimali fedha ili waweze kuzunguka nchi nzima kwa kukusanya saini zisipopungua milioni mbili za Watanzania kwa ajili ya kutimiza sharti la kufungua kesi.

Lengo la kesi hiyo ni katika mahakama ya kimataifa ni kudai fidia kwa kupiganishwa vita bila ridhaa yao.

Hayo yalisemwa na Malagila Shimba, mwenyekiti wa chama Cha Wazee Tanzania ambao walipigana Vita Kuu ya Pili ya Dunia kutoka Tanzania (TLC).

Kwa mujibu wa Shimba, uamuzi huo umefanywa na mkutano mkuu wachama cha askari hao.

Alisema waliopigana vita mwaka iliyomalizika 1945 ,wana nia ya kuifungulia kesi serikali ya Uingereza ,ili iweze kuwalipa fidia kwa kuwa walipiganidhwa Vita bila ridhaa yao, lakini pia haikuwa ridhaa ya Tanzania.

"Tunaomba serikali itusaidie rasilimali fedha ili tuweze kuzunguka nchi nzima kwa ajili ya kukusanya saini zisizopungua milioni mbili za Watanzania ili watimize sharti la kufungua kesho hiyo katika mahakama inayostahili," alisema.

# Wanawake wawezeshwa ushiriki uongozi na siasa

**Na Mary Geofrey**

CHAMA cha Wanahabari Wanawake (TAMWA) kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia wanawake (UN WOMEN), kimezindua mradi wa Uongozi na Ushiriki wa Wanawake katika Siasa.

Mradi huo utahusisha ufanyikaji wa midahalo ya habari, ili kuongeza uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa ushiriki wa mwanamke katika siasa na uongozi na madhara ya magonjwa ya milipuko kama COVID 19 kwa wanawake na wasichana.

Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Dk. Rose Reuben, alibainisha hayo jana, wakati akizungumza jijini Dar es Salaam akitambulisha kuanza kwa mradi huo utakaotekelezwa katika Mikoa 16, Wilaya 112 na Kata 458 nchini.

Aliitaja miongoni mwa mikoa hiyo ni Dar es Salaam, Morogoro, Pwani, Dodoma, Singida, Mbeya, Ruvuma, Lindi, Mtwara, Mwanza, Shinyanga, Mara na Tabora.

Alisema kwa mujibu wa ripoti ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ya mwaka 2016, inaonyesha kuwa asilimia 17 ya mawaziri ni wanawake, makatibu Wakuu ni asilimia 11, wakuu wa mikoa ni asilimia 23 huku wakuu wa wilaya wakiwa ni asilimia 28.

"Hali hii inadhihirisha namna nafasi ya mwanamke ilivyokuwa ndogo, licha ya hamasa zinazoendelea kufanywa na Serikali kwa kushirikiana na Asasi za Kiraia," alisema Dk. Reuben.

Kadhalika alisema kuwapo kwa mifumo kandamizi inayochochea ukatili kwa wanawake katika jamii, ndio sababu ya ushiriki duni wa wanawake kwenye nafasi za uongozi wa kisiasa na ngazi za uamuzi.

Kwa mujibu wa TAMWA, licha ya Serikali kuunda sheria zinazowaruhusu wanawake kushiriki nafasi hizo, bado kumekuwa na mwamko mdogo wa ushiriki wao kutokana na mifumo kandamizi iliyopo kwenye jamii dhidi yao.

Alisema mifumo hiyo inakinzana na azma ya kujenga jamii isiyokuwa na ubaguzi kama ilivyobainishwa kwenye dira ya taifa mwaka 2025, Katiba ya nchi ya mwaka 1977 na sheria mbalimbali.

Hata hivyo Dk. Reuben, aliipongeza Serikali kumteua Samia Suluhu Hassan kuwa Makamu wa Rais.



Meneja mwandamizi bidhaa za kidigitali na mauzo wa Benki ya NMB, Tito Mangesho (kushoto), akiwaelekeza walimu wa Kanda ya Ziwa, jinsi ya kujiunga na NMB mkononi App, wakati wa hafla ya Siku ya Walimu iliyofanyika mkoani Geita juzi, ambapo walimu zaidi ya 200 walishiriki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC Dar afurahia ujenzi wa barabara Kigamboni

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge, amelipongeza Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), kukamilisha ujenzi wa kipande cha barabara kinachounganisha Daraja la Nyerere na Kigamboni.

Aidha, amesema daraja hilo hutumika kama kivutio cha watalii kutoka nje na ndani ya nchi, ili kuongeza mapato ya Serikali.

Kunenge alisema hayo jana wakati wa ziara yake kukagua utekelezaji wa maagizo ya Rais Dk. John Magufuli kuhusu ujenzi huo.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, William Erio, alimueleza kuwa, ujenzi wa kipande hicho cha barabara ulikuwa umesimama kwa muda mrefu mpaka Rais alipotoa maelekezo Februari mwaka huu, wakati akifungua majengo ya Halmashauri ya Manispaa ya Wilaya ya Kigamboni.

Alisema kwa sasa ujenzi wa kipande hicho umekamilika kwa gharama ileile, na kwamba kazi inayofanyika ni kuweka alama mbalimbali za usalama barabarani, pamoja na kufunga taa za umeme wa jua 'solar' katika eneo hilo, ili kuliweka katika hali ya usalama zaidi na kuondokana na giza wakati wa usiku.

Kwa mujibu wa mkuu huyo wa mkoa, kutokana na muonekano mzuri wa daraja hilo, Serikali ya Mkoa wa Dar es Salaam, italifanya daraja hilo la Nyerere kuwa sehemu ya kivutio cha utalii kwa maana wakipata wageni kutoka nje ya nchi watawapeleka eneo hilo kama sehemu ya kufarijika na kuburudika.

Mhandisi Mkazi kutoka Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Simon Mgani, alisema ujenzi wa kipande hicho cha barabara ulikamilika Agosti 31, mwaka huu, na kwamba kwa mujibu wa mkataba wa ujenzi wapo katika kipindi cha mtazamo, ambacho ni cha miaka miwili.

Naye, Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, alisema ujenzi wa daraja na barabara hiyo ni uwekezaji mkubwa na mzuri wa Serikali na NSSF, na kuwataka wananchi kuilinda miundombinu hiyo.

# RC ataka mpango kukopesha walimu

**Na Happy Severine,**
BARIADI

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, ameomba kuanzishwa mpango mahusus kwa ajili ya wafanyakazi hasa walimu, ambao wamefika kiwango cha mwisho cha kukopesheka, utakao wasaidia kuacha kwenda kukopa katika taasisi zisizo rasmi.

Mtaka amesema kuwa, walimu wengi wamekuwa wakiweka rehani kadi zao za benki, kutozwa riba kubwa, pamoja na kunyang'anywa mali zao, pindi wanapokwenda kukopa katika taasisi ndogondogo za kifedha, ambazo siyo rasmi.

Mkuu huyo wa Mkoa alitoa ombi hilo wakati wa kongamano la siku ya Mwalimu (Teacher's day 2020) lililoandaliwa na benki ya NMB, ambalo limefanyikia mjini Bariadi na kujumuisha zaidi ya walimu 200 mkoa mzima.

Alisema kuwa ofisini kwake amekuwa akikutana na kesi nyingi za walimu kuchukuliwa mali zao, ikiwa pamoja na kukatwa riba kubwa kwenye mikopo, hali ambayo imewafanya walimu wengi kushindwa kufanya maendeleo.

"Walimu wengi kwa sasa wameona kukopa kwenye taasisi, ambazo siyo rasmi ni jambo la kawaida, wanaacha kadi zao rehani, lakini wamekuwa wakitozwa riba hadi asilimia 50, walimu wengi wanakopa akistaafu mafao yake yote yanaishia kwenye mkopo," alisema Mtaka.

Aliipongeza benki hiyo kwa kuanzisha utaratibu wa kukutana na wateja wao hasa walimu kwa ajili ya kusikiliza maoni yao, lakini pia kuwaleleza fursa mpya, ambazo zimeanzishwa na benki.

Aliwataka walimu kuacha tabia ya kwenda kukopa katika taasisi, ambazo siyo rasmi na badala yake watumie fursa, ambazo zinatangazwa na benki ikiwemo NMB katika kujiandaa na maisha ya kustaafu.

"Tumieni fursa hizi ambazo zinatangazwa na benki, kuhakikisha maisha yenu ya kustaafu yanakuwa mazuri, tumieni benki kukopa na siyo taasisi nyingine, ambazo zinawanyonya.

Hata hivyo benki hiyo ilikutana na walimu katika kongamano kama hilo Mkoa wa Geita, ambapo Mkuu wa Mkoa huo, Robert Gabriel alizitaka benki kutoa mikopo kwa walimu, ili waweze kuboresha maisha yao na kufanya kazi kwa uhakika kwa sababu ni waaminifu na wazalendo.

Meneja Mwandamizi wateja Binafasi wa Benki hiyo, Ally Ngingite, aliwataka walimu kukopa kwa malengo, ili kujiletea maendeleo yao wenyewe pamoja na familia zao, huku akiwataka kutumia fursa ya uwapo wa benki hiyo.

Badhi ya walimu walipongeza uboreshwaji wa mikopo ya nyumba, ambayo wameona kwao ni fursa kubwa kwa hivyo wanajipanga kuitumia na itawasaidia kwa ajili kujiandaa na maisha ya kustaafu.

"Jambo kubwa ambalo tumeliona na tumejifunza na tunakwenda nalo kama fursa, ni mikopo ya nyumba, kwa mara ya kwanza leo wamesema unaweza kupata mkopo wa kujenga nyumba kuanzia msingi, ," alisema Grace Julias Mwalimu Simiyu.

Naye Rosemary Malimi, mwalimu wa Shule ya Msingi Igenge Halmashauri ya mji wa Geita, alisema kuwa huduma hususani mikopo imemsaidia kusomesha watoto, bila usumbufu kwasababu benki hiyo inaruhusu kuongeza mkopo kama umeshafanya marejesho robo ya mkopo wa awali.



Mjumbe wa Kamati Kuu, Kassim Majaliwa, akiwahutubia wananchi katika mkutano wa kampeni eneo la Runzewe, Kata ya Uyovu, wilayani Bukombe, jana. **PICHA: OWM**

# Jamii yatakiwa kuripoti matukio ya ukatili

**Na Christina Mwakangale**

JAMII imetakiwa kutoa taarifa kuhusu matukio ya ukatili dhidi ya watoto, yanayotokea kwenye maeneo yao.

Naibu Msajili Mahakama Kuu ya Tanzania, Kitengo cha Watoto, Hakimu Nyigulila Mwaseba, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam kwenye semina ya ngazi ya jamii (GDSS), zinazofanyika kila wiki na kuandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

Mwaseba alisema taarifa hizo zinapaswa kutolewa kwa maofisa wa jamii, viongozi wa shule na kwenye halmashauri, ili kuondoa matukio ya ubakaji, ulawiti na ukatili wa watoto.

"Mahakama inafanya kazi kwa mujibu wa sheria, zipo sheria mbalimbali zinazohusika katika uendeshaji wa mashauri ya watu waliofanyiwa ukatili," alisema Mwaseba na kuongeza:

"Taarifa isipotolewa katika vyombo vya kisheria kuhusu ukatili wa watoto kijinsia ni kosa la jinai."

Changamoto zilizopo kwenye uendeshaji wa kesi hizo, alisema ni namna ya kupata taarifa kamili kuhusu tukio kutokana na watoto waliofanyiwa ukatili kupewa vitisho kutoka kwa watendaji.

"Sheria ya Mtoto sura ya 13 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2019. Ina vifungu ambavyo mtu anaweza kushtakiwa kwa kufanya ukatili kwa mtoto, akiwamo mtoto wa kike."

Mmoja wa washiriki wa semina hizo, Theresia Nyanjala, alisema elimu kuhusu namna ya kuripoti matukio hayo inahitajika kwenye jamii, kutokana na mila, desturi na woga uliopo kwa baadhi ya wahusika.

"Utakuta mzazi au mlezi anaogopa kwenda kutoa taarifa katika vyombo husika kutokana na kuona aibu katika jamii, elimu itolewe na ijulikane ni haki ya mtoto kutotendewa ukatili," alisema Nyanjala.

# Bil. 5.3/- kutekeleza miradi kuinua wanawake

**Na Elisante John, IKUNGI**

ZAIDI ya Sh. bilioni 5.3 zinatarajiwa kutekeleza mradi wa kuufikia usawa wa kijinsia kwa kuwawezesha wanawake na wasichana katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, mkoani Singida.

Pia, lengo ni wanawake hao kujikita kwenye kilimo cha alizeti na mboga, ili kuinua hali zao kiuchumi na kuzuia na kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia katika wilaya hiyo.

Mradi huo unatekelezwa kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) na Shirika la Umoja wa Mataifa la masuala ya wanawake na Shirika la Kimataifa la Maendeleo (KOICA) la nchini Korea.

Akizungumza juzi kwenye uzinduzi wa mradi huo utakaotekelezwa katika wilaya hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, alisema mradi huo utabadili mtizamo wa jamii hiyo kifikra.

Alisema, kwa hali ilivyo hivi sasa, ni dhahiri wanaume wamewachelewesha wanawake kwa muda mrefu katika kuboresha hali zao, hali iliyoodhoofisha mchango wa mwanamke katika maendeleo.

"Bila ya mfumo dume uliokuwapo, leo hii wanawake wangekuwa mbali sana kiuchumi, sasa ni lazima tubadilike na wanaume tambueni kuwa wanawake wanalo jukumu kubwa kuboresha uchumi wa familia... tuwape ushirikiano wafanye kazi za kujiongezea kipato," alisisitiza.

Awali, Mkurungezi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Justice Kijazi, alisema mradi huo utanufaisha wanawake 2,350, wa vijiji vya Kipumbuiko, Mnang'ana, Munyu na Irisya.

Alisema kuwa, ili lengo la mradi huo liweze kufikiwa, yatatolewa mafunzo ya kilimo bora cha alizeti na mboga, kwa ajili ya kundi hilo, kusambaza pembejeo za kilimo cha mazao hayo kwa mnufaika mmoja mmoja.

Uzinduzi huo, ulihudhuriwa na mwakilishi mkazi wa Umoja wa Mataifa hapa nchini, Zlatan Milisic na Msaidizi Mwakilishi wa UNFPA, Dk. Wilfred Ochan.

# CCM yaonya vijana kusubiri matokeo vyuoni

**Na Thobias Mwanakatwe**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimewatahadharisha vijana kutojiingiza kwenye mtego wa kusubiria matokeo kwenye vituo vya kupigia kura kwa sababu kufanya hivyo ni kwenda kinyume cha sheria.

Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Philip Mangula, alitoa tahadhari hiyo juzi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika kwenye uwanja wa ndege wa zamani jijini Mbeya.

"Wenzetu wameanza kuingia hofu, wanasema sisi tutaweka watu wa kulinda masanduku ya kura wakipiga kura wasitoke, sheria inawakataza, vijana tujihadhari tusiingie kwenye mtego, wakifanya vituko vyao tuende kutulia katika manyumba yetu," alisema.

Mangula alisema sheria inakataza kukaa kwenye kituo cha kupigia kura kinachotakiwa ukipiga kura nenda nyumbani kwa sababu kuna wakala ambaye anakuwa na jukumu la kuangalia kura za chama chako.

"Kituoni kutakuwa na mawakala 16 au 17 kulingana na vyama vinavyogombea, sasa wanaohamasishana eti wakalinde kura ili kuzuia wizi usitokee ni wawapi hawa, hofu imewaingia na mtu akiingiwa hofu anaweza kufanya jambo lolote," alisema.

Aidha, Mangula alisisitiza dhidi ya wananchi kuendelea kudumisha amani nchini hususani katika kipindi cha uchaguzi huu kwa kuwa bila amani hakuna maendeleo.

"Viongozi wetu tuendelee kuilinda amani yetu na wale wanaopingana na kubisha kila kitu nawashauri wangepinga kwanza na elimu bure ili watoto wao wasisome bure walipe," alisema.



Mtaalamu wa Kilimo kutoka Wizara ya Kilimo, Margaret Natai (kushoto), akimwonyesha Kaimu Ofisa Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Beda Chamatata (katikati), mazao yaliyozalishwa kwa kuongezewa virutubishi, wakati wa mkutano wa usambazaji wa mwongozo wa kitaifa wa uongezaji wa virutubishi kibailojia katika mazao ya chakula uliofanyika mkoani Shinyanga jana. Kulia ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Emmanuel Johnson. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kozi ya IATA yaanza kufundishwa NIT

**Na Prosper Makene**

MAMLAKA ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) imezindua mafunzo ya wakufunzi wa kozi za usafiri wa anga zinazoratibiwa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (IATA) kwa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT).

Kuzinduliwa huko ni mwanzo wa Chuo cha NIT kuanza kutoa kozi nne za usafiri wa anga ambapo zitaanza kutolewa katika mwaka wa huu wa masomo 2020/21.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Mkurugenzi Mkuu wa TCAA, Hamza Johari, aliupongeza uongozi wa chuo kwa jitihada kubwa walizozifanya hadi kukidhi vigezo vya kupata ithibati ya kuendesha kozi hizi nne muhimu zenye viwango vya kimataifa, na ni dhahiri kuwa Sekta ya Usafiri wa Anga sasa inaenda kukua kwa viwango vya kimataifa nchini."

Alisema Tanzania kwa muda mrefu imekuwa na upungufu mkubwa wa wataalamu katika sekta ya usafiri wa anga, lakini kupitia kozi hizi tatizo hili linaenda kupatiwa mwarobaini.

"Kozi hizi ni muhimu sana hasa katika kipindi hiki ambacho Serikali ya Awamu ya Tano imewekeza sana katika sekta ya uchukuzi ikiwapo sekta ndogo ya usafiri wa anga," alisema.

"Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu hii kutaongeza idadi na miruko ya ndege na huduma nyingine nyingi. Hivyo, mafunzo haya ni muhimu sana katika kuimarisha na kuboresha usafiri wa anga hapa nchini," alisema.

Naye Mkuu wa Chuo cha NIT, Profesa Zacharia Mganilwa, alisema "Chuo chetu kimepata ithibati toka IATA (Authorized Training Centre- ATC) kufundisha kozi nne ambazo ni (Airline Customer Service, Airline Marketing, Airport Operations Fundamentals pamoja na Global Distribution Systems Fares na Ticketing -Amadeus)".

Mkuu wa chuo hicho alisema mafunzo hayo yaliyozinduliwa wameanza kuyatoa kwa wakufunzi watakotumika kufundisha kozi za IATA nchini.

# 'Uandishi kitaaluma uwe shirikishi'

**Na Vincent Mpepo,** OUT

PROFESA Mugyabuso Mulokozi, amesema kuna haja kuwa na ushirikishwaji katika uandishi wa kazi za kitaaluma ikiwamo majarida, matini na vitabu ili kupata machapisho na kazi zinazokidhi viwango.

Profesa Mulokozi, mtumishi wa mstaafu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alitoa rai hiyo juzi wakati wa warsha ya uandishi wa makala, majarida na matini za kitaaluma inayofanyika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) jijini Dar es Salaam ikihusisha wanataaluma wa fani mbalimbali na watumishi wasio wanataaluma.

Alisema bado kuna tatizo katika matumizi ya lugha ya Kiingereza kimaandishi na kimazungumzo hususani katika vipengele vya kisarufi, msamiati, tahajia na taipografia.

"Kwa kufahamu au kutokufahamu, watumiaji wa lugha ya Kiingereza wanajikuta wanatumia Kiingereza cha Kimarekani au cha Uingereza, kitu ambacho hatuwezi kugundua kirahisi," Profesa Mulokozi alionya.

Alisema kuwa hata katika taaluma na uandishi wa habari kwenye uwanja wa masomo ya sayansi ikiwamo fizikia, botania, zoolojia na akiolojia, kuna kukosekana kwa umakini kufuata taratibu za uandishi na kwa kuzingatia uasilia wa lugha husika kwa uwanja husika.

Akichangia mjadala wa uandishi wa maandiko mbalimbali ya kitaaluma, Mhadhiri Evaristo Mtitu alisema mchakato wa uandishi ni kazi shirikishi inayohusisha wanataaluma wengi kwenye taaluma husika.

"Uandishi wa kitaaluma ni kazi shirikishi kwa kuwa hakuna kitu ambacho mtu binafsi anaweza kufanikisha," alisema Mtitu.

# Wastaafu waanzishiwa mpango

**Na Mwandishi Wetu**

WASTAAFU nchini wameandaliwa mpango maalum, unaolenga kuboresha maisha yao, ambao huenda ukawa ni mtatuzi wa changamoto mbalimbali ambazo huwa zinawakumba katika maisha ya ustaafu.

Chini ya mpango huo wenye kaulimbiu iitwayo 'Ndoto zako hazistaafu', unajumuisha fursa za kujiwekea akiba, uwekezaji na uwezeshaji wa kifedha kwa wastaafu.

Katika kufanikisha hilo, tayati zimeshazinduliwa huduma za akaunti maalum ya wastaafu iitwayo "Pension Account" na huduma ya uwezeshaji kifedha kwa wastaafu kidijitali "Pension Advance" kupitia huduma ya SimBanking App.

Hayo yalisema juzi na Ofisa Biashara Mkuu wa Benki ya CRDB, Dk. Joseph Witts, katika uzinduzi wa mpango huo na kwamba akaunti hiyo inawawezesha wastaafu kupokea pensheni zao kwa urahisi na usalama.

"Inasaidia pia kujiwekea akiba kutokana na vipato vinavyotokana na shughuli mbalimbali za kiuchumi wanazozifanya, na ili kutoa nafuu kwa wastaafu, akaunti hiyo hufunguliwa bure," alisema Dk. Witts.

Alifafanua kuwa haina makato yoyote na hutoa fursa kwa wastaafu kuunganishwa bure na mifumo ya utoaji huduma kidijitali ikiwamo SimBanking na Internet Banking.

"Ninajivunia kuwajulisha kuwa hadi leo hii tukiwa tunazindua mpango huu wa uwezeshaji wastaafu, tayari wastaafu zaidi ya 19,000 wameshafungua akaunti na wanafurahia huduma zetu," alisema .

Dk. Witts alisema, kupitia akaunti hiyo wastaafu wanapewa TemboCard inayowawezesha kupata huduma kwa CRDB Wakala na ATM zote nchini ikiwa ni njia ya kuwaondolea usumbufu.

Naye Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na Wakati wa CRDB, Boma Rabala, alisema kupitia mpango huo wa uwezeshaji kwa wastaafu benki hiyo pia imejipanga kuendelea kutoa mikopo kwa wastaafu.

# Mwongozo virutubishi kwenye mazao waja

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI imetoa mwongozo wa kitaifa wa uongezaji wa virutubishi kibailojia katika mazao ya chakula kwa ajili ya kupambana na changamoto zinazotokana na lishe duni nchini.

Mwongozo huo unasambazwa na Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Shirika la Nutrition International, inalenga kuwaongoza wadau katika shughuli zao za kuongeza mnyororo wa thamani ya mazao.

Hayo yalisemwa jana na Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Beda Chamatata, wakati akizungumza katika mkutano wa matumizi ya mwongozo wa wadau hao na kuwataka waunge mkono usambazaji wa mwongozo huo kupitia mipango na bajeti zao.

"Mwongozo huu utasaidia wadau wa sekta ya chakula kuzalisha vyakula vyenye virutubushi, ambavyo vitaboresha lishe katika jamii na kutuwezesha kufikia lengo letu la kumaliza utapiamlo unaosababishwa na ukosefu wa madini na vitamini," alisema Chamatata.

Alisema, asilimia 58 ya watoto nchini, wenye umri wa miezi sita hadi 59 na asilimia 45 ya wanawake wana upungufu wa damu, kulingana na Utafiti wa Viashiria vya Idadi ya Watu, Afya na Malaria wa mwaka 2015/2016.

"Mwongozo utaunganisha sekta ya kilimo na afya, na kuimarisha matumizi ya uongezaji wa virutubishi kibailojia katika mazao ya chakula, ambayo yatasaidia kuondoa changamoto ya upungufu wa virutubishi nchini," alisema.

# Bisanda: Teknolojia isaidie kuzalisha wahitimu bora

**Na Yusuph Nandonde,** OUT

MAKAMU Mkuu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), amezishauri taasisi za elimu ya juu nchini kutumia teknolojia katika ufundishaji, ili kuzalisha wahitimu wanaoendana na mahitaji ya nchi kuufikia uchumi wa viwanda.

Profesa Elifas Bisanda, aliyasema hayo juzi wakati akizindua baraza la chuo hicho ambalo ndiyo chombo cha juu katika uamuzi wa taasisi hiyo.

Profesa Bisanda alisema kufundisha kupitia mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kutasaidia kupata wahitimu wenye viwango bora kitaaluma huku pia ikisaidia taasisi hizo kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia.

"Taasisi nyingi zimehamia kwenye ufundishaji kupitia TEHAMA, kitu ambacho kinaonekana ni kigumu, lakini ni lazima tupitie mabadiliko hayo ili kuendana na mahitaji ya soko katika uandaaji wa wahitimu watakaokidhi vigezo", alisema.

Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Mitihani (OUT), Dk. Said Ali, alisema chuo hicho kilitathmini mabadiliko hayo mapema na kiliamua kufundisha na kutahini kwa kutumia mifumo ya TEHAMA, uamuzi ambao umekuwa na mafanikio makubwa.

"Mitihani kwa njia ya mazungumzo ipo duniani kwa miaka mingi, lakini mfumo wa kutoa maswali moja kwa moja kama tulivyofanya sisi ni kitu kipya na tunaweza kuwa wa kwanza katika hili," alisema.

# EWURA yawapa angalizo mafundi umeme

**Beatrice Moses,** TUDARCo

MAMLAKA ya udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imewaonya mafundi umeme, ambao hufunga mfumo wa umeme kwenye majengo mbalimbali.

Majengo hayo ni ya makazi, biashara na viwanda wakati hawana leseni, hivyo kushindwa kuzingatia mipaka na kanuni za kazi hiyo.

Kaimu Mkurugenzi wa Umeme EWURA, Mhandisi Nemes Victor Massawe, ameyasema hayo jana kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka hiyo, wakati akifungua mafunzo ya siku tatu ya mafundi umeme wa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

"EWURA imegundua kuwa miongoni mwenu kuna ambao hawazingatii miongozo iliyopo inayojumuisha sheria na kanuni katika utendaji wa kazi," alisema.

Mhandisi Massawe alisema wameandaa mafunzo hayo kwa lengo la kutoa elimu kwa mafundi hao, kwa kuwa wanatakiwa kufanya kazi kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizowekwa, ili kuimarisha usalama wa watu na mali zao.

Katika warsha hiyo EWURA iliandaa mafunzo ya vitendo yatakayosaidia kukumbusha au kupata uelewa juu ya upimaji wa vipimo mbalimbali, ambavyo mafundi hutakiwa kujaza kwenye fomu za watija wao za uombaji wa umeme zinazotolewa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Uamuzi wa kufanya hivyo ulifikiwa na mamlaka baada ya kukagua baadhi ya fomu, ambazo mafundi huwajazia wateja na kubaini hazijazwi kwa usahihi, hivyo EWURA inaamini mafunzo hayo yatasaidia katika kuleta tija zaidi huduma wanazozitoa.

"Ni matarajio yangu katika muda wa siku tatu mtakaokuwa hapa mtashiriki kikamilifu katika mada zitakazotolewa na wataalamu walioandaliwa, hatimaye mtakwenda kuboresha utendaji kazi wenu," alisema Massawe.

Mhandisi Evarist Simon wa EWURA alisema hadi sasa mafundi umeme wenye usajili ni 3284, idadi ambayo haijitoshelezi na mahitaji yaliyopo kwenye jamii.

Awali Mhandisi Ruta Kasabalala Kasabalala alisema, mafunzo hayo ni muhimu kwa kuwa yanasaidia katika kukumbusha au kuwajengea uwezo zaidi mafundi hao kuhusu wajibu wao katika utendaji wa kazi zao.



Wafanyabiashara wadogo wakiwa wamepanga biashara zao katika mtaro wa maji ya mvua na kwenye njia ya waenda kwa miguu, eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana, kitendo kinachosababisha msongamano mkubwa na usumbufu kwa watumiaji wa barabara hiyo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# RAS: Mafunzo ya PPRA yataokoa fedha za umma

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Tawala Mkoa wa Iringa, Happiness Seneda, ametoa wito kwa watendaji katika mkoa huo, kuhakikisha wanahudhuria mafunzo yanayotolewa na Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA) katika mkoa huo.

Akizungumza ofisini kwake alipotembelewa na wawezeshaji wa mafunzo kutoka PPRA, Seneda alisema kumekuwa na changamoto nyingi kwenye michakato ya ununuzi wa umma mkoani hapo, changamoto kuu ikiwa katika sehemu ya ujenzi, ambayo hutumia kiasi kikubwa cha fedha.

"Mafunzo haya kwa wanaohusika kwenye michakato ya ununuzi ni muhimu sana, hapa mkoani kwetu, kuna changamoto kubwa kwenye sehemu ya ujenzi, ambayo ndiyo inachukua thamani kubwa zaidi ya fedha. Changamoto kubwa zaidi ipo kwenye usimamizi wa mikataba," alisema.


Pia, alisema elimu kuhusu matumizi ya njia ya 'force account' katika zabuni za umma bado ni changamoto kuu katika mkoa huo kama ilivyo kwa maeneo mengine. Hivyo, aliishukuru mamlaka hiyo kwa kufika mkoani hapo kutoa mafunzo.

"Elimu kuhusu 'force account' bado ni changamoto. Baadhi ya watendaji hawana elimu ya kutosha kuhusu 'force account', hivyo inasababisha badala ya kupunguza gharama kama ilivyokusudiwa, imekuwa changamoto," alisema Seneda.

Naye Ofisa Ununuzi Mwandamizi - Mafunzo na Ushauri kutoka PPRA, Gilbert Kamunde, alimshukuru kwa ushirikiano wake katika kuwahamasisha watendaji na kuona umuhimu wa mafunzo hayo. Alisema mamlaka inaamini mafunzo hayo yatasaidia katika kuongeza ukidhi wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 na marekebisho yake ya mwaka 2016 na kupata thamani halisi ya fedha kwenye kila ununuzi wa umma.

PPRA iliendesha mafunzo ya siku tatu mkoani humo kuanzia Septemba 30 hadi jana, ambayo yalitolewa bure kwa watendaji kupitia programu maalum yamepangwa kufanyika katika mikoa 10, ndani ya kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021.

"Kwa kweli mafunzo haya yamekuwa na tija sana kwetu watendaji, ninaamini itasaidia kupunguza au kuondoa kabisa baadhi ya makosa yalikuwa yanafanyika kutokana na uelewa mdogo wa sheria. Pia, itapunguza sana hoja za ukaguzi na itaongeza uwajibikaji," alisema Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Iringa, Juliana Mkalimoto.




Ukurasa 13

Safari ya kura za 'mafiga matatu'

BUFE

IJUMAA OKTOBA 1, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 12

**KATIBU MKUU MALIASILI: Hii ndio bucha ya nyamapori na mpango mkuu itakavyoendeshwa**

UCHUMI

# Wahitimu sekondari wanaoondoka na zawadi stadi elimu ya ujasiriamali

**Na Yasmine Protace, Mkuranga**

UJASIRIAMALI unatajwa kuwa ni uwezo wa akili na ubunifu wa mtu kutambua fursa ya kuiendea fursa, kuipangia mkakati na hatimaye kuthubutu na kuiweka katika uhalisia.

Hapo kunamaanisha kuzalisha bidhaa yenyewe na kisha inatafutiwa masoko, ikifanywa itambulike kwa watumiaji. Kimsingi, imekuwa mkombozi kwa makundi mbalimbali yanayoinuka kiuchumi.

Uzoefu unaonyesha hadi sasa kuna kundi la watu wanaojiingiza katika kufunza ujasiriamali, lengo ni kujiongezea kipato cha umma.

Hivi karibuni Shule ya Sekondari ya Victory iliyopo wilayani hapa, imeanza kuwafundisha wanafunzi ujasiriamali katika lengo la kusaidia kujiongezea kipato, wakiwa majumbani.

Mbali na kujiingiza kipato, ujasiriamali huo watakaoufanya, utawasaidia kwa kuwajibika kila mara, ikiwamo kutoendeleza ukaaji vijiweni.

Mkuu wa shule hiyo, Ponsiano Mlelwa katika Mahafali ya 13 ya Kidato cha Nne, anafafanua kuwa: "Tumeona ni vyema kuanzia masomo ya ujasiriamali kwa wanafunzi, lengo ni kuwasaidia kujiongezea kipato wakirudi majumbani."

Mwalimu Ponsiano anaongeza kuwa, ujasiriamali waliojifunza utawasaidia wanafunzi kuwa na muda zaidi masomoni na hawatojiingiza katika makundi yasiyofaa.

Kwa mujibu wa mkuu wa shule huyo, taratibu zote zaa uongozi shuleni zilifutawa, hadi kuandaa vifungashio kamili vikiwamo nembo za bidhaa zinazozalishwa hali hapo.



Mgeni rasmi (katikati), akikagua bidhaa iliyotengenezwa na wahitimu wa kidato cha nne, katika Shule ya Sekondari Victory. **PICHA: YASMINE PROTACE.**

**WALICHOJIFUNZA**

Ponsiano anasema wanafunzi wamejifunza kutengeneza sabuni za vyooni, katika masinki na mafuta ya kupaka, pia jinsi ya kupiga picha, kukiwapo zaidi ya wanafunzi 100 wanaotarajiwa kumaliza kidato cha nne, kukiendana na ujuzi huo.

Ofisa Elimu Taaluma wa Mkoa Pwani, Hildegard Makundi, anaipongeza shule kwa kuwafundisha wanafunzi ujasiriamali, kwani unatarajiwa kuinua uchumi wa familia wanakotoka majumbani na wanakuwa mbali na maisha ya kushinda vijiweni.

Makundi anawataka wazazi wa wahitimu kuwapatia mitaji watoto wao watakaporudi majumbani, ili waendeleze ujasiriamali huo kwa manufaa yao.

"Wazazi mmeona watoto wamepata elimu ya ujasiriamali kinachotakiwa muwapatie mitaji kidogo ili waendeleze kuzalisha vitu walivyofundishwa, ambavyo vitawainua kimaisha, ikiwamo familia kujiongezea kipato," afafanua Makundi.

**WAHITIMU?**

John Msaki, mwanafunzi ambaye ni mhitimu mtarajiwa wa kidato cha nne katika shule hiyo, anasema somo la ujasiriamali kwake litakuwa mkombozi katika maisha yake.

Anakiri kujifunza kutengeneza sabuni ya maji inayotumika kusafishia choo na masinki, pia anafafanua amejifunza kutengeneza mafuta ya kujipaka, yote yanafungua mtazamo wa kujiongezea kipato.

"Nimejifunza nimeelewa nikimaliza shule, muda wangu nitatumia kutafuta masoko kwa ajili ya kuanzia kuuza bidhaa ambazo nitakuwa natengeneza," anasema Msaki.

Kijana huyo anakiri amefundishwa utengenezaji bidhaa zitakazamuongezea kipato na hatakuwa na muda wa kushinda vijiweni arudipo, rai yake wazazi wawawezeshe mitaji ya kutengeneza bidhaa.

Hanifa Jumanne, anasema elimu hiyo imemfikia wakati sahihi, kwamba amejipanga watakapomaliza mitihani na kurudi majumbani, wataanza kujisajili kupitia kazi za mikono, kwani mafunzo waliopatiwa yamewaweka pazuri kuanza kuyatumia.

"Tumejifunza ujasiriamali kutengeneza sabuni na mafuta ya kupaka,tumeweza kuvitengeneza. Hivyo, sasa tunaporudi nyumbani, tutayatumia mafunzo katika kujizalishia kipato," anasema.

Anaongeza kuwa muda wa kujiegesha ndani ndani kusubiri matokeo ya mtihani sasa umekwisha, badala yake ni suala la uzalishaji bidhaa walizofunzwa, ili ziwe mkombozi kwao katika uchumi wa familia.

Juma Jumanne, ni mwanafunzi aliyejifunza kupiga picha, jambo analoamini lina nafasi ya kuongezea kipato na dira yake ni atakaporudi nyumbani, atajituma kuwaomba fedha wazazi kununua kamera na baada ya hapo anatafuta masoko akajikite katika kazi ya upigaji picha.

BIASHARA

## KATIBU MKUU MALIASILI:

# Hii ndio bucha ya nyamapori na mpango mkuu itakavyoendeshwa

- Leseni mwezi huu ikianzia mikoa 23
- Wazo la miaka 20, hofu ilikuwa ujangili
- Bei 'dezo'; mbegu itafika kila mahali

**Na Christina Haule, Morogoro**

WIZARA ya Maliasili na Utalii, sasa inaanika msimamo wake kwamba kuanzishwa bucha za kuuza nyamapori, sio tu kutatoa fursa ya ajira na kuongeza kipato, pia kutasaidia upatikanaji nyamapori kwa Watanzania wapendao kitoweo hicho.

Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Aloyce Nzuki, anasema pia ni uamuzi utakaopunguza ujangili unaotokana na jamii kupendelea kula nyamapori, hivyo kudhibiti ushawishi wa biashara haramu ya bidhaa nyamapori.

Dk. Nzuki anasema, wizara imeshafanya maboresho ya kanuni za ufugaji wanyamapori katika mashamba, ranchi na bustani, kwa kupunguza bei za wanyama wa mbegu.

Anasema hiyo inawalenga ili wananchi wamudu gharama za ufugaji kwa kuwa ufugaji wa wanyamapori ndio chanzo kikuu cha nyama itakayouzwa kwenye mabucha.

Katibu Mkuu anasema, wizara imepunguza bei za wanyama wa mbegu kwa asilimia 90, ili wananchi wamudu gharama za ufugaji mashambani katika ranchi na bustani za wanyamapori zitakazoanzishwa Tanzania Bara, kuwezesha uhakika wa kupatikana nyamapori za kuuza kwenye bucha hizo.

"Kwa mfano, bei ya wanyamapori kama nyati imepungua kutoka Sh. milioni 4.1 hadi Sh. 210,000; Swala na Pala kutoka Sh. 300,000 hadi Sh. 90, 000," anaeleza.

Anataja vyanzo vingine vya upatikanaji nyamapori, ni uwindaji wa kitalii na kienyeji na wageni wakazi.

Uwindaji kitalii mara nyingi huchukua vitu mbalimbali na nyama zinapobaki, hufikishwa kwa wananchi kupitia bucha zilizoanzishwa.

**MAUDHUI YAKE**

Dk. Nzuki anataja mikoa 23 kati ya 26 nchini, itaanza kutoa huduma za bucha za nyamapori, Zikiwamo Songwe, Mara na Rukwa na itaongezeka baada ya kukamilika utaratibu wa kiutendaji.



Biashara ya nyamapori buchani ikiendelea katika baadhi ya nchi inakofanyika. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Katibu Mkuu huyo ameitaja mikoa itakapopatikana bucha za nyamapori Dar es salaam, Morogoro, Tanga, Pwani, Singida, Dodoma, Tabora, Katavi, Kigoma, Shinyanga, Geita, Kagera, Mwanza, Simiyu, Iringa, Mbeya, Njombe, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Manyara, Arusha na Kilimanjaro.

Anasema wizara imeweka vigezo vya magari maalum yatayotumika kubeba na kuuza nyamapori na yatapatiwa leseni za kutoa huduma za usambazaji na uuzaji nyama kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Dk. Nzuki anasema, mpaka sasa walishapokea jumla ya maombi 25 ya wananchi wanaokusudia kuanzisha bucha za nyamapori, yatakayopitiwa na kamati maalum na inatarajia kukutana Oktoba 12 ijayo na kutoa leseni za uanzishaji mabucha hayo.




Wizara ya Maliasili kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), ilipokea maelekezo ya kuanzisha bucha za nyamapori kutoka kwa Rais Dk. Magufuli, mnamo Januari 3 mwaka huu, alipokuwa ziarani mkoa wa Rukwa.

Anasema, ni fursa inayoendana na matakwa ya Sera ya Wanyamapori ya Mwaka 2007 na Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori, inayohimiza wananchi kutumia na kunufaika moja kwa moja na shughuli za utalii.

Katibu Mkuu anasema, shughuli za utalii zinailetea serikali kupitia matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori, ambazo sekta utalii inachangia asilimia 25 ya fedha za kigeni. Anaeleza sera inayoongoza sekta ndogo ya wanyamapori nchini ya mwaka 2007, inaitaka serikali kuhakikisha sekta ya maliasili inazidi kuimarika na kuendelea kutunza maliasili za nchi, mazao yatokanayo na maliasili kuchangia ukuajI uchumi kitaifa.



Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Aloyce Nzuki

Dk. Nzuki anataja mazao ya misitu na nyuki yanawaongezea wananchi kipato na kufungua fursa za ajira.

**BUCHA INAVYOAZISHWA**

Anafafanua kuwa, kila mtu anayekusudia uanzisha bucha za kuuza nyamapori, anatakiwa kuwasilisha maombi ndani ya siku 14 kuanzia Septemba 25 iliyopita kwa Kamishna wa Uhifadhi Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA).

Hiyo inafanyika kupitia ofisi zake zilizoko jijini Dar es Salaam, Arusha na Morogoro na Dk. Nzuki anasema uuzwaji nyamapori katika bucha zitakazopata leseni, utakuwa ni wa soko huria, zikiuzwa kulingana na nguvu ya bei ya soko kwa wakati huo.

**IDARA YA UTALII**

Naibu Kamishna wa Uhifadhi Huduma za Utalii na Biashara, Imani Nkuwi, anasema TAWA imewaonya wanaofikiri kuanzishwa kwa bucha za nyamapori, ndio njia ya kufanya ujangili, kwani wamejipanga kudhibiti na kusimamia hilo kisheria.

Nkuwi anasema TAWA imejiandaa kikamilifu kuhakikisha fursa hiyo inatumiwa kikamilifu kwa malengo yaliyokusudiwa na sio kijangili. "Tunao askari wenye magwanda na wasio na magwanda, ambao watakuwa na kazi ya kufuatilia na kukamata watakaofanya ujangili na kuchukuliwa hatua za kisheria. Anasema, wizara tayari imeshakamilisha kanuni za biashara ya bucha za nyamapori, ikiwamo kutambua zitakapopatikana nyama, sambamba na njia bora za ufugaji wa wanyamapori hao.

Nkuwi anasema, pia wamejipanga kusimamia na kudhibiti biashara ya wanyamapori kwa usalama wa afya ya mlaji na kanuni itazingatia, kwa wauzaji buchani, wenye ranchi au bustani za wanyama na madaktari mifugo watakaopima na kuhakikisha uchinjaji salama.

"Kwa kufuga wanyamapori, wataweza kutibu wanyama hao sababu kisheria wafugaji wa wanyamapori hao, lazima waajiri atakayepima na kutibu wanyama wanaofugwa," anasema Nkuwi.

Anamhakikishia usalama kiafya kila mlaji nyama hiyo, kwa kuzingatia kanuni zilizowekwa na atakayeuza nyamapori, anawajibika kuthibitisha alikopata.

Nkuwi anasema, wazo la uanzishaji mabucha ya nyamapori lilikuwepo tangu mwaka 1988, wazio lililohamishiwa katika Idara ya Wanyamapori, lakini wazo lilisitishwa mwaka 1989, kutokana na kasi ya ujangili kitaifa.

**VIKWAZO VILIVYOPO**

Kaimu Kamishna wa TAWA, Mabula Misungwi, anasema kinachowakwaza ni vibali vya kuwa tozo kubwa ya ukamataji nyama wa mbegu, kutoka kampuni binafsi zenye taaluma za kukamata wanyama hao porini.

Anasema, kutokana na hali hiyo, TAWA ilijipanga na kukutana na kampuni hizo kujadili namna ya kupunguza gharama hizo kutoka kiasi wastani wa Sh.milioni nne hadi mbili, ili kufanikisha azma.

Misungwi anaendela: "Licha ya kwamba mkamataji naye anaangalia 'riski' atakayoipata kwenye kukamata wanyama, mfano mkamataji hawezi kumkata simba kama ambavyo angeweza kumkamata twiga.

"Ni lazima kutakuwapoa gharama tofauti, kutokana na athari ambazo kama asipokuwa makini, zinaweza kutokea kwake. Lakini, anapaswa kuangalia usawa na hali ya soko anayokwenda kukutana nayo kwa sasa," anaeleza Misungwi.

Anaeleza kuwapo uwezekano wa kuwapo bei kubwa ya ukamataji wanyama wa mbegu porini, unaotokana na idadi ndogo ya wahitaji wa wanyamapori hao.


**WANANCHI NA LAO**

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wakazi wa mkoa Morogoro, Ashura Ibrahimu, anaelekeza shukurani kwa serikali kupitia wizara husika, kwa kuanzisha uuzaji nyamapori kwenye bucha, jambo analolieleza litawawezesha bila tabu wananchi, hata wasiowahi kula nyama hizo.

"Wapo wananchi ambao mpaka sasa wana umri mkubwa wa kuzaliwa, lakini hawajawahi kula nyamapori, wala hawajui ladha ya nyamapori yoyote, zaidi ya kusikia kuwa nyama ya swala tamu, nyama ya pofu tamu...kwa kweli wengi tutafaidi" anasisitiza.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Safari ya kura za 'mafiga matatu'






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
jkulangwa@yahoo.com

WATANZANIA wanaendelea na kampeni kwa ajili ya kupata viongozi wao wa miaka mingine mitano. Leo hii, pilika za kampeni zinasikika na kushuhudiwa huku na kule nchi nzima, wagombea kwa ngazi zao wakijinadi kwa kuambatana na timu zao.

Hiyo ni baada ya serikali inayoongozwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kumaliza kipindi chake cha miaka mitano kwa mujibu wa Katiba ya nchi.

Upo uwezekano wa CCM kuunda serikali nyingine kwa miaka mitano ijayo, hali kadhalika, upinzani nao unaweza kuunda serikali mpya na kuing'oa CCM madarakani na kuweka historia mpya, baada ya CCM iliyotokana na Afro Shiraz Party (ASP) na Tanganyika African National Union (TANU).

Tambo za hapa na pale zinaendelea, lakini mwenye siri ni mpiga kura ambaye atajilawa asubuhi ya Oktoba 28 kutekeleza haki yake ya kikatiba, ya kujichagulia viongozi anaowataka. Atakuwa anamchagua Rais, Mbunge/Mwakilishi na Diwani.

Katika mikutano yote ya kampeni, wagombea wanatoa ahadi zao, huku wale wa CCM wakitambia utekelezaji wa ahadi walizozitoa mwaka 2015 na upinzani wakiahidi watafanya nini wakipewa fursa hiyo, nao wakitafuta matobo ya utekelezaji kwenye ahadi za CCM.

Upole, ukarimu na maneno matamu kutoka kwa wagombea, ndivyo vimetamalaki sambamba na ahadi ambazo kwa kauli inaweza kuaminika, kuwa zitatekelezwa hasa kutokana na ushawishi wa utekelezaji wao, jambo ambalo ni sharti lisubiriwe kuonekana.

Hakuna mgombea, mathalan atakayekubali kutoa ahadi ndogo na kushindwa kuwahakikishia wapiga kura kuwa itatekelezwa ndani ya kipindi chake cha miaka mitano ijayo.

Hivyo, ni jukumu na wajibu wa mpiga kura kusikiliza na kuchekecha na kuona uwezekano wa ahadi husika kutekelezwa.

Pia, ni wajibu na jukumu la mpiga kura kumuelewa mgombea zaidi, badala ya chama chake ambacho ndicho mtunga sera na kumwachia mtekelezaji atekeleze. Ina maana kwamba, yawezekana kuwa na sera nzuri, lakini zikakosa mtekelezaji sahihi.

Vyama vyote vilivyosimamisha wagombea katika maeneo yote matatu, vinaamini katika Utatu Mtakatifu au Mafiga Matatu.

Imani hiyo, inavifanya viombe wapiga kura kuchagua mafiga hayo, hata kama moja au mawili ni bovu au mabovu.

Kuna wakati inatokea mafiga (mawe) mawili imara na lingine likawa laini, lisiloweza kuhimili moto au sufuria lililoinjikwa.

Ndivyo inavyokuwa pia katika siasa, kwamba mgombea urais anaweza kuwa mzuri, mbunge mzuri, lakini diwani hafai na kinyume chake.

Nadharia hiyo inaweza kusababisha mpiga kura akachagua rais wa chama kingine tofauti na cha mbunge na diwani, ili mradi atambue sifa zao kiutendaji.

Ni bahati nzuri Watanzania tunafahamiana kitabia, kiuwezo na hata kiakili na hasa wale tunaoishi katika maeneo ya pamoja, mathalan jimboni au kwenye kata. Mbunge au diwani ni rahisi zaidi kujua tabia yake.

Hasa katika viongozi wetu wa ngazi za chini, umma wa wapiga kura umekomaa kwa kiasi chake na kwa kiasi kikubwa, ukakumbatia zaidi ya itikadi ya kuchagua mtu kwa kuangalia sifa na uwezo aliyo nao, jambo linalovifanya vyama kuwa makini katika uteuzi wa wagombea wao.


Kama anavyohimiza Rais John Magufuli, maendeleo huwa hayana chama. Hivyo, watakaokiuka dhana ya mafiga matatu, kwa kiasi kikubwa wahusika mara nyingi ni waliosimamishwa katika nafasi hizo.

BIASHARA

# Kampeni zilizopambwa na ahadi zinazomfariji mkulima shambani

## • Mawese, chai, kahawa, tumbaku, miti

**Na Nebart Msokwa, Mbeya**




Zitto Kabwe.




Tundu Lissu.



Prof. Ibrahim Lipumba.



Dk. John Magufuli.

SHIRIKA la Kilimo na Chakula Duniani (FAO), linakitaja kilimo kuwa sekta muhimu duniani, likichangia wastani wa asilimia 15 ya pato la taifa kwa nchi moja moja na ndiye mlishaji mkuu wa watu bilioni 1.3 barani Afrika.

Nchini Tanzania, inatakwa kuajiri wastani wa theluthi mbili ya wakazi wake, hivyo kuwa sekta inayoongoza kuajiri idadi kubwa ya wananchi, kwa ajira za moja kwa moja na zisizokuwa za moja kwa moja.

Kwa kurejea taarifa ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), sekta hiyo inachangia asilimia 24 katika Pato la Taifa na asilimia 30 ya mapato yatokanayo na mauzo ya nje ya nchi.

Kutokana na umuhimu wake, wagombea wa nafasi ya urais wa vyama mbalimbali vya siasa nchini wameifanya kuwa ajenda muhimu kwenye mikutano ya kampeni kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.

Wanasiasa hao kwa nyakati tofauti wamesikika kwenye mikutano yao ya kampeni, wakijinasibu kuwa endapo watachaguliwa na wananchi, watahakikisha wanaboresha sekta hiyo ili wanufaike nayo.

**KUTOKA CCM**

Akiwa mkoani Tabora, mgombea urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, anawahakikishia wakulima wa tumbaku nchini, kwa ahadi kuwa endapo atachaguliwa kuongoza nchi kwa miaka mingine mitano, atahakikisha anatatua changamoto za zao hilo.

Anazitaja baadhi ya changamoto hizo, kuwa ni pamoja na ukosefu wa soko la zao hilo, kutokana na wanunuzi kuwa wachache na wanunuzi kuchelewesha malipo.

Dk. Magufuli, anasema pamoja na bei ya tumbaku kuporomoka, pia hali hiyo ilitokea kwenye mazao mengine ya biashara kama korosho na pamba na kwamba tatizo lilisababishwa na mlipuko wa virusi vya Corona duniani, uliosababisha wanunuzi kutoka nje kusitisha kuja nchini kununua.

Pia, alipokuwa mkoani Kigoma, Dk. Magufuli, mwalimu wa hisabati na somo la kemia, alilozama nalo katika ngazi zote tatu za shahada ya chuo kikuu, anaahidi serikali yake kufufua michikichi mkoani Kigoma.

Anasema katika hilo, pia atafufua yaliyokuwa mashamba ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), hivyo akawataka wananchi kulima.

Mgombea Mwenza wa Dk. Magufuli, Samia Suluhu Hassan, katika ziara yake mkoani Mbeya, anaahidi chama kuanzisha viwanda vya kuchakata mazao mbalimbali ya kilimo, ili kuwawezesha wakulima hao kupata soko la mazao stahiki.

Vilevile, anasisitiza kuwa serikali wanayokusudia kuiunda inalenga kununua ndege ya mizigo itakayowasaidia wakulima kusafirisha mazao yao kwenda kwenye masoko ya nje, badala ya kutumia ndege za kigeni.



Mkulima wa tumbaku akiwajibika shambani. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**JICHO LA CUF**

Mgombea urais kwa tiketi ya Chama cha Wananchi (CUF), msomi wa uchumi, Profesa Ibrahim Lipumba, naye yumo katika safari kujinadi, akielekeza mtazamo zaidi wa kuchochea uzalishaji mashambani, iwapo atafanikiwa kushinda nafasi hiyo kwenye uchaguzi wa mwezi huu.

Akiwa wilayani Uyui katika mkoa wa asili yake Tabora, Profesa Lipumba, anasema endapo atashinda uchaguzi na kushika nafasi hiyo, atahakikisha serikali yake inawatafutia wakulima wa tumbaku soko la kimataifa.

Anasema soko kubwa la tumbaku duniani lipo nchini China, anakodai panaongoza duniani kwa kuwa na wavutaji zaidi ya milioni 400, hivyo anawasisitiza wakulima waendelee kulima zao hilo kwa bidii.

Upande wa zao la pamba, Profesa Lipumba, anasema serikali yake itahakikisha inaanzisha viwanda vya nyuzi na nguo, ili wakulima waongeze uzalishaji na wanufaike kutokana na uwepo wa soko hilo.

Anasema atahakikisha viwanda vyote vya nguo vilivyokufa vinafufuliwa, ili wakulima wa pamba wapate soko la uhakika ndani ya nchi badala ya kutegemea soko la nje pekee.

Profesa Lipumba, katika mzunguko wake wa kampeni jijini Dodoma, anawaahidi wakazi kuwa serikali yake itaboresha kilimo cha zabibu, kwa kuwawezesha wakulima kuzalisha kisasa, huku akidai kuwa atawatafutia soko kwa njia ya mtandao.

Anasema, endapo zao hilo litalimwa kisasa na wakulima watapata soko la uhakika, litakuwa moja ya mazao yatakayowaondoa wananchi wa Mkoa wa Dodoma kwenye umaskini.

Safari yake mkoani Kagera, Prof. Lipumba, anajinadi na hoja yake haja ya kuwa na uchumi wa soko, kwamba atakapofanikiwa kuzipata zinazomuweka madarakani, serikali yake itawatafutia wakulima wa kahawa soko la kimataifa na la uhakika, ili wanufaike nalo, akidai itakuwa tofauti na ilivyo sasa hivi.

Mbali na maeneo ya Kagera ambako zao hilo linalimwa kwa kwa sehemu kubwa ya mkoa, zao hilo pia lipo katika wilaya kama Mbinga (Ruvuma), Rungwe (Mbeya) na Mbozi (Songwe).

Profesa Lipumba anasisitiza ilani ya CUF inaelekeza Serikali kuwasaidia wakulima wadogo kulima kilimo cha kisasa na kuwatafutia masoko ili kuwa na uhakika wa chakula na kipato.

**CHADEMA JE?**

Mgombea wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu, anatangaza ilani katika kampeni kwamba, atakapoposhinda kwenye kinyang'anyiro cha kuwania urais mwaka huu, atawaboreshea mazingira wakulima wanufaike na shughuli hiyo.

Tundu Lissu, anaahidi kuzitumia rasilimali zilizopo mkoani humo, ikiwamo chai na mazao ya miti, kuinua uchumi wa wananchi walioko hapo.

Lissu, anaahidi kubadilisha mfumo wa utawala ili rasilimali za maeneo ziwanufaishe wananchi wa eneo husika, hasa kwa kutumia mfumo wa majimbo.

Akiwa mkoani Kagera, Lissu ambaye ni mtaalamu wa Sheria na Makamu Mwenyekiti wa Chadema, alisema serikali yake itahakikisha wakulima wa kahawa wanauza mazao yao kuuzwa kokote pasipo kuzuiliwa na serikali.

Lissu anawaahidi wakulima kufaidi nguvu zao, kwa kuuza kwa bei nzuri, itakayoendana na gharama za uzalishaji, tofauti na ilivyo sasa.

Akiwa mkoani Mbeya, Lissu alifafanua serikali yake itakuwa na utaratibu wa kuwawezesha wakulima na wafanyabiashara wa mazao kuuza mazao watakapokuwa wamepata soko zuri.

**ACT- WAZALENDO**

Agosti 30 mwaka huu, Chama cha ACT - Wazalendo kilifanya uzinduzi wa Ilani yake ya Uchaguzi ya mwaka 2020/2025 jijini Dar es Salaam, ilipobainisha mambo makuu 11 ya kipaumbele, ambayo serikali yake itayatekeleza endapo kitapata ridhaa ya kuongoza nchi.

Katika hilo, kilimo kimo katika orodha ya vipaumbele vikuu kwa kuhakikisha kinaboreshwa kwa kuanzisha ushirika wa kisasa kwenye sekta hiyo muhimu.



# TARI yataja mikoa mitatu kutikisa soko la korosho

**Na Ashton Balaigwa,** DODOMA

WATAFITI wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Kituo cha Naliendele cha mkoani Mtwara, wamebainisha mikoa ya Dodoma, Singida na Morogoro kuonyesha dalili ya kuzalisha korosho bora ambazo zitatikisa soko la dunia.

Dalili hizo zimetokana na uzalishaji wa awali uliofanywa na wakulima wa mikoa hiyo kuonyesha ubora wa hali ya juu huku wakiwa hawana elimu yoyote ya kilimo hicho.

Akizungumza jana katika mafunzo ya kilimo hicho kwa wakulima wa wilaya za Chamwino na Chemba zilizopo mkoani Dodoma, Mtafiti wa zao la korosho, Kasiga Ngiha, alisema kupitia korosho za awali zilizozalishwa na wakulima hao, wamebaini kuwa korosho zinazopatikana kwenye ukanda wa kati zitakuwa na bora zaidi ya zile za mikoa ya Kusini.

"Tulitarajia kuwa korosho zilizozalishwa na wakulima hawa ambao hawajapata elimu yoyote ya kilimo bora zitakuwa hazina ubora, lakini kama tulivyojionea wanazo korosho bora na hii ni dalili kuwa wakulima hawa wakipata elimu watazalisha korosho bora zaidi ambazo zitahimili ushindani wa soko la ndani na nje ya nchi hivyo kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zinazozalisha korosho bora zaidi duniani," alisema Ngiha.

Alisema mikoa hiyo ina hali ya hewa na mazingira mazuri kwa kilimo hicho na wakiongeza juhudi kwa kuhudumia vizuri mashamba yao watalibeba taifa.

Ngiha alisema kwa sasa TARI kupitia kituo chake cha Naliendele wanatoa mafunzo ya kilimo bora cha korosho kwenye mikoa yote 17 inayolima zao hilo nchini ili kusambaza teknolojia ya kilimo cha zao hilo na kuongeza uzalishaji.

Naye, mkulima wa zao hilo wilayani Chamwino, Athanas Mkambe, alisema kuwa alianza kilimo hicho miaka minane iliyopita na hakuwahi kupata elimu yoyote.

"Nilishaanza kuvuna korosho na wataalam hawa wanasema ni korosho bora, vikwazo nilivyokabiliana navyo ni magonjwa ya mimea hali hii imekuwa ikisababisha nipate mavuno kidogo kulingana na ukubwa wa shamba langu," alisema.

"Mimi na shamba lenye mikorosho zaidi ya 250, lakini nimekuwa nikivuna korosho chache kutokana na kukosa elimu ya namna ya kudhibiti magonjwa kwenye mikorosho yangu, lakini kwa elimu ambayo nimeipata kwenye mafunzo haya naamini sasa nakwenda kuhudumia vizuri shamba langu."

Kwa upande wake, Mwakilishi wa Bodi ya korosho nchini, Ray Mtangi, alisema licha ya wakulima hao kuzalisha korosho kwa kiwango kidogo, kutokana na ubora wake watapata soko la uhakika lililopo jijini Dodoma.

"Wakulima wetu hawa bado wanazalisha korosho kwa kiwango kidogo ambacho sio rahisi kuwaleta wanunuzi kutoka nje ya nchi kuja kununua mazao yao ambayo yanaweza yasifike hata tani moja, lakini kutokana na ubora wa korosho zao, wakulima hawa wakiungana wakaunda vikundi na kuzibangua wanaweza kuziuza kwenye hoteli za kitalii ambayo ni mengi sana hapa Dodoma," alisema Mtangi.

Hata hivyo, Mtangi alisema kuwa endapo wakulima hao wataongeza uzalishaji na kufikia angalau kuanzia tani 50 kuna uwezekano wa wanunuzi kutoka nje ya nchi kufika Dodoma kununua korosho.




Meneja wa Benki ya Posta Tanzania (TPB), Mkoa wa Dodoma, Shaban Telatela (kushoto), akikata keki pamoja na baadhi ya wazee wa mkoa wa huo, jijini Dodoma jana kuadhimisha Siku ya Wazee Duniani na kuenzi mchango wa wazee katika benki hiyo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Sampuli za udongo kupimwa kusaidia wakulima

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Kilimo imesema itahakikisha inapima sampuli za udongo kwenye wilaya zote nchini ili kuwasaidia wakulima na wawekezaji kujua virutubishi gani na aina ipi ya mbolea au zao la kupanda.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Gerald Kusaya, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akisaini mkataba na Taasisi ya kujenga mapato vijijini kupitia ujasiriamali (BRITEN), ili kuendeleza sekta ya kilimo.

Alisema tayari Kituo cha Utafiti wa Kilimo (TARI) Selian cha Arusha, kimekusanya sampuli za udongo kwenye kata zote 3,956 za Tanzania bara ili kujua aina gani ya zao inastahili na mbolea ya kutumia ili kuwa na uhakika na kilimo.

"Tunahitaji tabia za udongo ziwe wazi na kuwezesha wakulima na wawekezaji kujua eneo la kwenda kulima na aina gani ya zao na pembejeo za kutumia," alisema.

Akizungumzia kuhusu mkataba huo, Kusaya aliagiza iundwe kamati ndogo ya wataalam wa wizara itakayofanya kazi ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mkataba uliosainiwa na mingine ya aina hiyo.

Alisema hatua hiyo inalenga kuimarisha ujuzi wa biashara kwa wakulima wadogo ili kufanya kilimo biashara na kutunza mazao kabla na baada ya mavuno.

Alisema mkataba huo utasaidia wizara kutumia fursa ya kuongeza ujuzi kwa wakulima pia matumizi ya teknolojia na kuwapatia mbinu bora za kuongeza kipato.

"Tunataka kupitia ushirikiano huu na BRITEN tuwasaidie wakulima hususan wadogo kuongeza kipato, usalama wa chakula ili sekta ikue zaidi na kuongeza tija na pato la taifa," alisisitiza Kusaya.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa BRITEN, Josephine Kaiza, alisema Shirika lao limebobea kwenye utekelezaji wa miradi ya kilimo, kibiashara na kutengeneza ushindani wa kibiashara kwa kuwafundisha wakulima mbinu za uzalishaji bora wa mazao.

Josephine alitaja mafanikio ya taasisi hiyo kuwa ni kuongeza muunganiko wa wadau wa sekta ya kilimo kufanya kazi kwa pamoja na kugusa maisha ya wakulima 165,000 mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

"Tunaamini kupitia makubaliano haya tutaweza kuchangia maendeleo ya kilimo kwa ufanisi zaidi na kufikia wakulima wengi zaidi," alisema.

## Waomba kuongezwa kliniki wagonjwa selimundu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHAMA cha Madaktari na Wagonjwa wa Mangonjwa yasiyo ya kuambukiza (TANCDA), kimeiomba serikali kuongeza kliniki kwa ajili ya wagonjwa wa selimundu ili kupata matibabu kwa haraka.

Mwenyekiti wa chama hicho ambaye pia ni Rais wa Chama cha Madaktari nchini Dk. Elisha Osati, alitoa ombi hilo juzi jijini hapa wakati akitoa taarifa kuhusu ziara walioifanya katika mikoa ya Kanda ya Ziwa hivi karibuni.

Dk. Osati alisema katika mikoa hiyo wamebaini kuwapo kwa kliniki mbili licha ya kuwa na idadi kubwa ya wagonjwa katika maeneo hayo.

"Tunaomba serikali iangalie namna ya kuongeza kliniki za wagonjwa wa selimundu lengo wote wapate tiba pamoja na elimu ya kujukinga na ugonjwa huo," alisema Dk. Osati.

Vile vile, alisema wamepima wanafunzi 10,000 na watoto 3,600 kati ya hao 1,800 wamekutwa na chembechembe za selimundu.

"Licha ya idadi kuwa sio kubwa sana, lakini tunaamini kuna walio na chembechembe za ugonjwa huu na hawajitokezi kupata matibabu," alisema.

Mwenyekiti huyo aliomba serikali kushirikiana na jamii kupiga kampeni ya kutokomeza na kuwatafuta wagonjwa wenye selimundu ili kupata matibabu katika vituo mbalimbali vya afya.

"Huu ugonjwa upo na watu wengi wanaonekana kutoujua vizuri ndio maana hawajitokezi kupata matibabu, hivyo wenye uelewa ukimuona mtu au mtoto mwenye dalili hizo mpe ushauri wa kwenda hospitali," alisema Dk. Osati.

Mkurugenzi Msaidizi wa magonjwa hayo kutoka Wizara ya Afya, Dk. Charles Kiologwe, alisema Tanzania inashika nafasi ya nne kwa kuwa na idadi kubwa ya wagonjwa wa selimundu.

Aliahidi kufanyia kazi ombi la chama hicho ili kudhibiti ugonjwa huo kuenea kwa jamii.

Alisema hatua muhimu zilizochukuliwa ni pamoja na kuweka mpango mkakati wa kuhakikisha ugonjwa huo unadhibitiwa kuanzia 2020-2025 na kliniki zinaanzishwa ili kutibia wagonjwa pamoja na kutoa elimu.

"Serikali inachukulia uzito mkubwa suala la ugonjwa huu wa selimundu, hivyo litashughulikiwa vilivyo na serikali," alisema Dk. Kiologwe.





# Vijana wapewa siri kujikwamua kwenye umaskini

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

VIJANA wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, wametakiwa kuitumia elimu waliyopatiwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kituo cha Uyole jijini Mbeya ili kujikwamua na umasikini kupitia sekta ya Kilimo kwa kuhakikisha wanaongeza uzalishaji kwa kulima mazao yenye tija.

Hayo yalisemwa juzi na Mkurugenzi wa Kituo hicho, Dk. Tulole Bucheyeki wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya siku tano kwa vijana 90 kutoka katika mikoa ya Iringa, Mbeya na Songwe.

Dk. Bucheyeki alisema lengo la kuwapatia vijana hao elimu ya kuzalisha mbegu bora ni kuhakikisha tatizo la ukosefu wa mbegu kwa wakulima linatatuliwa na kuweza kuongeza uzalishaji wa mazao yatakayo saidia kuinua uchumi wa kati.

Alisema vijana hao watapatiwa elimu mbalimbali ambazo ni Utafiti wa Udongo, Utafiti wa mbegu bora za mahindi, Maharage, Soya, Ulezi, Matunda mbalimbali, zao la pareto.

"Tumeamua kufanya hivi kwa lengo la kuhakikisha vijana wanapata ajira na kutatua changamoto ya wakulima kutumia mbegu feki wakati uwezo wa kuzalisha mbegu bora upo na vijana hawa wanauwezo mkubwa," alisema Dk. Tulole.

Naye mtafiti kutoka kituo hicho, Chrispin Mlowe, alisema Taasisi hiyo itatoa mafunzo hayo kwa awamu tatu ambapo zaidi ya vijana 300 watapatiwa elimu hiyo na kuhakikisha wanakuwa wakufunzi kwa wananchi.

Alisema wakulima wanatakiwa wazalishe kwa kufuata utaratibu wanaoelekezwa na wataalamu wakiwamo maofisa kilimo wa vijiji, vijana hao waliopatiwa elimu hiyo pamoja na wataalamu wanaouza pembejeo za kilimo.

Alisema taasisi hiyo haitaki watu kuendelea kujiita wakulima wadogo wakati teknolojia zipo nyingi na kwa sasa hivi wamekuja na teknolojia ya kupima udongo na kuwashauri wakulima mazao yanayofaa kulingana na aina ya virutubisho.

"Kwa sasa serikali imefanikiwa kuingia kwenye uchumi wa viwanda na kwamba kuna unahitaji malighafi za kutosha kwa ajili ya viwanda vinavyoendelea kuanzishwa, sasa tukiendelea kuwa na wakulima wadogo wengi haitatusaidia," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wakulima katika maeneo mbalimbali kuzalisha mazao ya kimkakati kwa kutumia mbegu za kisasa zinazozalishwa na taasisi hiyo ili wainuke badala ya kuendelea kuwa vile vile huku baadhi wakitumia mbegu za kienyeji.

Baadhi ya vijana walioshiriki mafunzo hayo walisema watakuwa wakufunzi kwa wakulima wenzao ilikuweza kuhakikisha sekta ya kilimo inakuwa na kuwainua kiuchumi.

Mmoja wa vijana hao kutoka Halmashauri ya Busokelo, Hamis Mwakyusa, alisema elimu aliyopewa itakuwa ni msaada mkubwa kwake kuweza kuhakikisha anajiajili na kusaidia wakulima huko vijijini.

# Wenye ulemavu wakumbukwa uchaguzi mkuu

**Na Nebart Msokwa na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imesema imeandaa utaratibu maalumu wa kuwawezesha watu wenye uhitaji maalumu wakiwamo wenye ulemavu kushiriki kupigia kura wakati wa uchaguzi mkuu Oktoba 28, mwaka huu bila kikwazo cha aina yoyote.

Akizungumza jana wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa wadau wa Uchaguzi mkoani Mbeya, Mjumbe wa NEC, Asina Omari, alisema katika kila kituo cha kupigia kura, kutakuwa na kifaa cha maandishi ya Nukta Nundu kwa ajili ya watu wasioona hasa wanaojua kukitumia kifaa hicho.

Alisema kwa watu wenye ulemavu wa kuona ambao hawajui kuvitumia wataruhusiwa kwenda na watu wanaowaamini kwa ajili ya kuwasaidia kupigia kura.

"Kwa wenye ulemavu wa viungo vituturi (vyumba maalumu vya kupigia kura) vina pande mbili ambazo upande mmoja ni mrefu na huu ni kwa watu wa kawaida na kikigeuzwa kinakuwa kifupi kumwezesha mwenye ulemavu huo wa viungo kupiga kura," alisema Asina. Vilevile alisema kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi, kwenye vituo vya kupigia kura watapewa kipaombele watu wa makundi maalumu ambao ni walemavu, wazee, wagonjwa, kinamama wanaonyonyesha na watakaoenda kwenye vituo wakiwa na watoto wao.

Aidha alisema Tume inawashirikisha wadau wa uchaguzi ili kuhakikisha shughuli hiyo inafanyika kwa amani na utulivu huku akiwaomba wadau kuhakikisha elimu inatolewa kwa wananchi wanaoshirikiana nao.

Flora Mkama, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Uchaguzi, aliwaomba wagombea wa nafasi mbalimbali kwenye uchaguzi huo pamoja na wafuasi wa vyama vyao kuzingatia maadili ya uchaguzi ili kuepuka kuharibu utaratibu.

Alisema wakati wa kuandaa kanuni za maadili ya uchaguzi, vyama vyote vilishirikishwa kutoa maoni na kwamba maadili hayo yanasimamiwa na kifungu cha Sheria ya uchaguzi namba 124A sura ya 343.

Alisema wagombea pamoja na vyama vyao, walipewa fomu namba 10 ya tamko la kuheshimu na kutekeleza maadili ya uchaguzi na kwamba walisaini fomu hizo siku ya uteuzi na hivyo wanatakiwa waendelee kuheshimu maadili hayo. "Tume inasisitiza wagombea kuepuka matumizi ya lugha za kashfa, maneno ya uchochezi yanayotishia usalama na amani ya nchi, pia wanatakiwa kuepuka kufanya kampeni zinazoashiria ubaguzi katika misingi ya jinsia, ulemavu, ukabila, udini, maumbile na rangi," alisema Mkama.

Mwakilishi wa Mkuu wa Idara ya Uhamiaji Mkoa wa Mbeya, Inspekta Sophia Mlimakifi, alisema watu pekee wanaostahili kupigia kura ni raia wa Tanzania ambao wamejiandikisha kupigia kura na kwamba raia wa kigeni hawatakiwi kushiriki.

Alisema wakati wa uandikishaji maofisa wa uhamiaji walikuwa wanafuatilia kazi hiyo kwa kushirikiana na maofisa watendaji pamoja na wananchi kuhakikisha kila anayeandikishwa ni Mtanzania.

Hata hivyo baadhi ya watu wenye ulemavu waliipongeza tume kwa kuwaandalia mazingira mazuri ya kushiriki kazi hiyo ikiwemo kuandaa vifaa vya kuwasaidia watu wenye ulemavu wa kuona.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (wa pili kushoto), akiwa pamoja na baadhi ya viongozi wa dini wa mkoani humo, wakifanya maombi maalumu kwenye Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa huo hivi karibuni, ambalo linaendelea kujengwa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wauzaji, wasambaza mbegu waonywa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Udhibiti wa Mbegu nchini (TOSCI), imetahadharisha kampuni zinayouza na kusambazaji mbegu kuacha kuwauzia wakulima mbegu feki kwa maelezo kuwa vitendo hivyo vinawaingiza wananchi hasara.

Mkaguzi wa mbegu kutoka TOSCI Makao Makuu jijini Dodoma, Dk. Mngotosha Ngomuo, alitoa tahadhari hiyo juzi jijini Mbeya wakati wa maofisa wa taasisi hiyo kutoka makao makuu pamoja na wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini walipofanya ukaguzi wa kawaida wa mbegu kwenye maduka mbalimbali yanayouza pembejeo.

Alisema mfanyabiashara atakayekamatwa anasambaza mbegu hizo atachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani kwa maelezo kuwa vitendo hivyo vinafifisha juhudi za serikali kuinua kilimo.

Alizitaja mbegu ambazo zinatafsiriwa ni feki ni ambazo hazijakaguliwa na mamlaka hiyo na kuwekwa nembo, zilizopitwa na muda wake pamoja na zinaingia nchini kupitia njia za panya kutoka mataifa mengine.

"Kuna mbegu imeingia nchini kinyemela ikitokea nchi jirani ya Zambia, mbegu hiyo inasemekana inapatikana mkoa wa Songwe hasa Wilaya ya Mbozi, nawaomba wananchi kuwa makini kwa kuzichunguza mbegu hizo kabla ya kwenda kupanda ili kujiridhisha," alisema Dk. Ngomuo.

Alisema kwenye ukaguzi huo walibaini mbegu nyingi zinazouzwa kwenye maduka zimepitwa na wakati na hivyo wakaziondoa ili wafanyabiashara hao wasiendelee kuzisambaza.

Mkaguzi wa mbegu kutoka Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mary Kilawe, aliwataka wadau kushiriki kuzuia usambazaji wa mbegu hizo kwa akiwataka kutoiachia TOSCI peke yake.

Alisema usambazaji wa mbegu feki una madhara makubwa kwa wakulima ikiwemo kuwasababishia wakulima hasara ya kutovuna kabisa mazao kama ambavyo wanakuwa wamekusudia.


Aliwataka wauzaji wa mbegu hizo kuwa wazalendo kwa kuhakikisha wanaepuka kusambaza mbegu hizo huku akidai kuwa wao ni wasimamizi wa sheria na hawapendi kuwachukulia hata wafanyabiashara na ndiyo maana wanatoa elimu.

"Tunajitahidi kutoa elimu ili wananchi hawa wasivunje sheria, sasa tukimkuta mtu ambaye tuna uhakika ana elimu lakini anauza mbegu feki tafsiri yake inakuwa kwamba anafanya makusudi hivyo lazima tumchukulie hatua hali," alisema Kilawe.

Baadhi ya wafanyabiashara wa mbegu jijini mbeya waliishukuru taasisi hiyo kwa kufanya ukaguzi huo wakidai kuwa unasaidia kuwakumbusha baadhi ya kanuni na taratibu za uuzaji wa mbegu.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Yusta Mraki, alisema baadhi ya wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu ndio wanaoichafua shughuli hiyo kwa kuwafanya hata waaminifu waonekane hawafai.

Aliwaomba maofisa hao kuendelea kuwatembelea mara kwa mara hasa kipindi hiki cha kuelekea msimu wa kilimo ili kutoa elimu zaidi na kuzuia uuzwaji wa mbegu ambazo hazikidhi vigezo.



# ZEC yazishauri asasi kuelimisha wapigakura

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC), imezitaka asasi za kiraia zilizopewa kazi ya kutoa elimu kwa wapiga kura kuifanya kazi hiyo kwa ufanisi mkubwa wakijua kwamba wapo baadhi ya watu hawafahamu haki za msingi za kupiga kura.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa ZEC, Jaji mstaafu Hamid Mahmoud, wakati akizungumza na asasi za kiraia zilizoteuliwa kusimamia kazi ya kutoa elimu kwa wapigakura, Unguja na Pemba.

Alisema ZEC imeziamini asasi hizo kwamba zinao uwezo wa kuifanya kazi hiyo na elimu kuwafikia wananchi wengi kabla ya siku ya kupiga kura.

"Naziomba asasi za kiraia zilizopewa kazi ya kutoa elimu kwa wapiga kura kuifanya kazi hiyo kwa uadilifu mkubwa na kufikia malengo yake ili wananchi wafike siku wakifanya uamuzi sahihi wa kuchagua viongozi wao," alisema.

Mkurugenzi wa ZEC, Thabit Faina Idarous, alisema maandalizi ya uchaguzi yamekamilika kwa asilimia kubwa na sasa kazi kubwa ambayo Tume imezipa asasi za kiraia ni kutoa elimu kwa wapigakura.

"Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kazi kubwa imefanya ya maandalizi ya uchaguzi mkuu wa Oktoba ambapo kwa sasa kwa upande wa asasi za kiraia kutoa elimu kwa wapigakura ili wananchi wafanye uamuzi sahihi," alisema. Akizungumza kwa niaba ya Mrajisi wa asasi za kiraia, Mwanasha Saleh Sheha, alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanawafikia wananchi mbalimbali ikiwamo vijijini kwa ajili ya kutoa elimu ya uraia kuhusu uchaguzi mkuu na kupiga kura.

"Tunazitaka asasi za kiraia zilizopewa kazi ya kutoa elimu kufikisha ujumbe huo vizuri kwa kuwataka wananchi wafahamu haki ya kidemokrasia kuchagua viongozi wanaowataka," alisema.

Ali Juma, ambaye amepata kazi ya kutoa elimu kwa wapigakura, alisema amejipanga kufikisha elimu hiyo katika baadhi ya visiwa ikiwamo Tumbatu ili wananchi wachague viongozi wenye maslahi ya kuleta maendeleo.

"Nimejipanga kutoa elimu ya wapigakura ambapo mimi nimekusudia kufikisha ujumbe katika visiwa vidogo ikiwamo Tumbatu, Mkoa wa Kaskazini Unguja," alisema.



Mgombea Uwakilishi wa jimbo la Tunguu kupitia CCM, Simai Mohamed Said, akihutubia wananchi katika uzinduzi wa kampeni za jimbo hilo, kwenye uwanja wa Mwarabu, Kibele Zanzibar jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Viongozi wa dini watakiwa kuhimiza amani kwa waumini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

VIONGOZI wa dini wakiwamo maimamu wa misikiti wametakiwa kuhimiza amani na utulivu kwa waumini wao ili kuhakikisha amani inadumu katika kipindi chote cha uchaguzi.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Khamis Juma Mwalimu, wakati akizungumza na viongozi wa dini ikiwamo maimamu katika misikiti ya Mkoa wa Kaskazini Unguja. Alisema viongozi wa dini wana wajibu mkubwa wa kuhimiza amani na utulivu kwa sababu wanasikilizwa na wafuasi wengi katika nyumba za ibada.

"Tunaelekea katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu, tunawaomba viongozi wa dini katika nyumba za ibada kuhimiza amani na utulivu ili nchi iwe salama," alisema.

Naye Katibu wa Mufti Mkuu wa Zanzibar, Khalid Mfaume, aliwataka Maimamu kutumia hotuba za sala ya Ijumaa kwa ajili ya kufikisha ujumbe wenye mnasaba wa kujenga na kuimarisha amani katika kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu. Aliwataka viongozi wa msikiti ikiwamo kamati kuacha kuwaruhusu watu kutoa mawaidha yenye kuhamasisha jazba za kisiasa na kusababisha vurugu.

"Viongozi wa kamati za misikiti tunawaomba wadhibiti nyumba za ibada na kamwe wasikubali kutumika kwa ajili ya mawaidha yatakayosababisha chuki na kuelekea vurugu za kisiasa," alisema.

Imamu wa msikiti wa Mkwajuni uwanjani, Shekhe Ali Issa alisema, wamejipanga vizuri kuzitumia hotuba za sala ya Ijumaa kwa ajili ya kuwajenga kimawazo vijana kupenda amani na kuepuka chuki zitakazowaingiza katika vurugu.

"Tumetoa hotuba mbili mwezi uliopita ambazo zote zimejikita katika kuwajenga vijana tabia njema ikiwamo uvumilivu kwa kumlaani shetani aliyelaaniwa na Mwenyezi Mungu," alisema.

# Jamii yaaswa kuficha vitendo vya ukatili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MTANDAO wa kupinga ukatili, udhalilishaji wa kijinsia Wilaya ya Wete Pemba, Mkoa wa Kaskazini, umetoa elimu kwa wanajamii 2,667 mwezi wa Agosti hadi Septemba, mwaka huu huku asilimia 54 waliofikiwa ni wanawake.

Miongoni mwa wanamtandao hao, Seif Sharif Makame, alisema katika kipindi hicho wamefanikiwa kuibua na kufuatilia kesi nane, kati ya hizo nne zinahusu matukio ya ubakaji.

Aliitaka jamii kuacha kuficha matukio ya udhalilishaji wa kijinsia na kutoa taarifa katika vyombo vya kutunga sheria likiwamo jeshi la polisi.

"Bado lipo tatizo la jamii ya Wazanzibari kuficha matukio ya vitendo vya ukatili wa kijinsia na kuvisuluhisha kwa njia ya kifamilia...tukificha matukio hayo hayatamalizika na yataleta athari kubwa mbele ya jamii zetu," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya wazazi, Asha Juma Omar, alisema baadhi yao hawana nafasi ya kusikiliza matatizo ya watoto na wakati mwingine huwa chanzo cha matatizo.

"Tunawataka wazazi waishi karibu na familia zao kwaajili ya kuyapatia ufumbuzi matatizo yanayowakabili wazazi...watoto wanatakiwa kusikilizwa matatizo yao tusiwe wakali mbele ya watoto," alisema.

Ofisa tathmini na ufuatiliaji wa TAMWA Zanzibar, Mohamed Khatib, aliwataka wanamtandao hao kuendelea kuzifuatilia kwa ukaribu kesi zilizoibuliwa ili kuona zinafikishwa mbele ya vyombo vya sheria.

Alisema kazi za mitandao ya udhalilishaji wa kijinsia sio kufuatilia kesi hizo pekee, lakini pia kuziibua na kuona zinafikishwa mbele ya mahakama kwa ajili ya kusikilizwa.

"Faida za kuwapo kwa mitandao ya kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia tumeziona ambazo ni kuibua kesi na kuzifuatilia kwa karibu ili zifikishwe mbele ya mahakama na kutajwa," alisema.

Mratibu wa TAMWA huko Pemba, Fat-hiya Mussa Said, alisema jamii imeanza kubadilika na kutoa taarifa za matukio hayo katika vyombo vya sheria pamoja na wengine kufika katika ofisi za chama hicho kwa ajili ya msaada wa ziada.

"Mafanikio ya kuwapo kwa mitandao ya kijamii ya kutoa taarifa na kufuatilia matukio ya vitendo vya ukatili wa kijinsia tumeyaona...wananchi toeni taarifa za matukio ya ukatili wa kijinsia ili wahusika wafikishwe mbele ya vyombo vya kisheria kwa hatua zaidi," alisema.

## MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA/MASHAMBA

**BEACH PLOT FOR SALE**
PLOT SIZE: - 0.91 Acres (3682.64 Square Meters)
LOCATION: - PLOT NO 40, KUNDUCHI BEACH, NEXT TO SILVER SANDS,DARESALAAM CITY
DESCRIPTION: - DIRECT ACCESS TO THE BEACH.
INTERESTED BUYERS MAY CONTACT +255 753786114

### VIWANJA/MASHAMBA

**Eneo linapangishwa/kuuzwa**
Eneo linapangishwa/ kuuzwa ukubwa wa mita mraba (sqm) 3,130, Tabata Liwiti, Dar es Salaam. Liko katika barabara kuu na inafaaa kwa ajili ya kujenga kituo cha mafuta, super market nk. Wasiliana kwa simu: 0715624747/0767235965.

### VIWANJA/MASHAMBA

**PRIME PLOT FOR SALE**
PLOT SIZE: - 14.87 HECTARE (36.74 ACRE)
LOCATION: - BAGAMOYO DISTRICT, BLOCK C SANZALE, LOCATED ON MAIN ROAD, 5 MIN FROM BAGAMOYO TOWN,3 KM AWAY FROM ROUND ABOUT
DESCRIPTION: - THE PLOT IS FURTHER DIVIDED IN 5 DIFFERENT TITLES.
INTERESTED BUYERS MAY CONTACT +255 753786114

*NIPASHE NI JIBU LAKO*
NJOO UTANGAZE NASI
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

### KUPOTEA KWA CHETI



115916702

**Hafsa Idrisa Mtamike** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha nne chenye index namba **S.0491/0020** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2014 katika shule ya Sekondari Kilomeni. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/KIJ/RB/707608/2020**

### KUPOTEA KWA CHETI



115925702

**Khadija Seif Luwongo** anatangaza kupotelewa kwa cheti ya kidato cha nne chenye index namba **S.1599/0075** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2011 katika Shule ya Sekondari Baobab. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/TAB/RB/13223/2020**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FARIDA MJILI MGUDE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA IST** yenye namba za usajili **T101 DKG,** iliyotolewa na mamlaka ya mapato Tanzania.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/MAG/RB/704966/2020**

115925202

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ELIZABETH GASPER MHINA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA CORONA YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 353 AWF.** CHASSIS NAMBA **ATZ100025575.** YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/BUG/RB/674601/2020.**

215925402

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDEKIRO ASSERI MAIMU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TRACTOR** yenye namba za usajili **T 237 CFN.** Chassis **No. 2199810,** Engine **No.087023N.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/RB/6089/2020.**

115925602

### KUPOTEA KWA CHETI



115925102

**Grace John Kisunge** anatangaza kupotelewa kwa Transcript ya kidato cha sita chenye index namba **S.1599/0715** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2020 katika shule ya Sekondari Baobab. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/TAB/RB/707014/2020**

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**PAULINUS RAPHAEL MSIGWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 270 AVW.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu Taarifa **MBE/MBE/R-B/707068/2020.**

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**STEPHEN SAULO MAPOLU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **Toyota Harrier** yenye namba za usajili **T 842 DEK** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi **MBE/MBE/R-B/706616/2020**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Mahakama ya Mwanzo MAKOLE WILAYA YA DODOMA**

**MADAI NAMBARI 889/2020**

**MDAI.................HILDA PHILEMON KIRA**

**DHIDI YA**

**MDAIWA....................RAYMOND PIUS NYENZA**

**KWA RAYMOND PIUS NYENZA**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba MADAI YA PESA TSH.1,200,000/=**

115925502

Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya JUMATATU tarehe 05/10/2020. saa 2:00 asubuhi kwa kujibu madai na kwa kuwa siku hiyo ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashidi *wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angalia kama *hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama ikithibitisha kama *umepokea kuitwa shaurinihii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 24/09/2020

Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;272/2020**

**Ombi la RASHID SHABANI ALLY,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SHABANI ALLY GELEZA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 13/10/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 01/10/2020.

Tarehe 1/10/2020

Sahihi ya Hakimu

215925802

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Papa Francis akataa kuonana na waziri

**VATICAN, Italia**

VATICAN imemkatalia Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo kuonana na kiongozi wa Kanisa Katoliki duniani, Papa Francis.

Kiongozi huyo wa juu wa Kanisa Katoliki ameelezwa kuwa hawapokei wanasiasa wakati wa kipindi cha uchaguzi.

Hatua hiyo inaongeza hali ya mzozo wa kidiplomasia baada ya kauli ya Pompeo kuhusu China na Kanisa Katoliki.

Vatican ilimshutumu Pompeo kuwa anajaribu kutumia suala hilo kuvutia wapigakura wa uchaguzi wa urais wa mwezi Novemba nchini Marekani.

Katika makala ya mwanzoni mwa mwezi Septemba, Pompeo alisema kanisa Katoliki linapoteza mamlaka yake ya kinidhamu kwa kufanya makubaliano mapya na China kuhusu uteuzi wa maaskofu.

Rais Donald Trump anapata uungwaji mkono kutoka kwa mashirika ya kidini ya kihafidhina, pamoja na wapigakura wa kikatoliki wa kihafidhina, ambao wengine wanadhani Papa Francis ni mtu mwenye uhuru.

Makundi ya haki za binadamu yanasema kuwa Wakatoliki wengi nchini China wanateswa kwa kuahidi utii kwa Papa badala ya chama rasmi cha Wakatoliki nchini China.

Pamoja na hayo, mnamo 2018 Vatican ilifanya makubaliano na China kuwa na maoni kuhusu uteuzi wa maaskofu wa China.

Wakati huo, Papa Francis alisema alikuwa na matumaini kuwa mpango huo utaruhusu vidonda vya zamani kupona na kuleta umoja kamili wa Kikatoliki nchini China.

Makubaliano hayo yanatarajiwa kufanywa upya mwezi ujao kukiwa na upinzani kutoka kwa Wakatoliki wengine, pamoja na Marekani.

Katika hotuba yake Jumatano huko Roma, Pompeo aliitaka Vatican kutetea uhuru wa kidini nchini China, akisema hakuna mahali popote palipo na uhuru wa kidini unaoshambuliwa zaidi ya China.

Wanadiplomasia wa juu wa Vatican, Waziri wa Mambo ya Nje, Kadinali Pietro Parolin na Waziri wa Mambo ya Kigeni, Askofu Mkuu, Paul Gallagher, alisema Papa Francis hatampokea Pompeo.

"Papa aliweka wazi kabisa kuwa wanasiasa hawatapokelewa katika kipindi cha uchaguzi. Hii ndiyo sababu, Kadinali Parolin alisema, kwa mujibu wa shirika la habari la AFP.

Wanasiasa wawili pia wamegusia ukosoaji wa hadharani wa Pompeo dhidi ya Papa Francis kama jambo la kushtusha na Askofu Mkuu Gallagher alisema kuwa masuala ya mjadala yanapaswa kuzungumzwa faragha.

Kardinali Parolin pia alisema inawezekana kauli ya Pompeo imelenga kuwahamasisha Wakatoliki kumuunga mkono Trump katika kura za mwezi Novemba.

"Wengine wametafsiri kwa njia hii kwamba maoni yalikuwa juu ya matumizi ya kisiasa ya nchini Marekani. Sina uthibitisho wa hii lakini kwa hakika hii ni njia moja ya kuiangalia," alieleza.

Aliongeza kuwa mpango wa Vatican na China hauhusiani na Marekani.

***BBC***



Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis. **PICHA: MTANDAO**

# Mwanaharakati Belarus ashinda tuzo ya Nobel

**STOCKHOLM, Sweden**

MWANAHARAKATI wa haki za binadamu nchini Belarus, Ales Bialiatski (BILIASKI) ametangazwa kuwa mmoja wa washindi wanne wa tuzo mbadala ya Nobel inayotolewa kila mwaka na wakfu wa Right Livelihood wa mjini Stockholm.

Ales na shirika la haki za binadamu aliloasisi liitwalo Viasna wametambuliwa jana kwa mchango mkubwa wa kudai demokrasia na haki za binadamu nchini Belarus, ambako kwa wiki kadhaa waandamanaji wanapinga matokeo ya uchaguzi wa Rais uliofanyika mwezi Agosti.

Mshindi mwingine wa tuzo hiyo ni mwanasheria kutoka Iran Nasrin Sotoudeh aliyewatetea wanaharakati, wanasiasa wa upinzani na wanawake walioshtakiwa kwa kosa la kutovaa hijab.

Washindi wengine wawili wa tuzo hiyo ni mwanasheria wa haki za kiraia wa nchini Marekani, Bryan Stevenson pamoja na mwanaharakati wa masuala ya mazingira kutoka nchini Nicaragua, Lottie Wren.

***DW***

## Viongozi EU kutafuta suluhu Mediterrania

**BRUSSELS, Ubelgiji**

VIONGOZI wa mataifa 27 wanachama wa Umoja wa Ulaya wamekutana jana mjini Brussels kutafuta njia ya kumaliza mvutano unaongezeka kati ya Uturuki na wanachama wawili wa kanda hiyo Ugiriki na Cyprus.

Mvutano huo ni kuhusiana na shughuli za utafutaji gesi katika eneo la mashariki ya Mediterannia.

Duru kutoka mjini Brussels zimearifu kuwa ingawa mkutano huo utajumuisha ajenda nyingine muhimu, suala la Uturuki litakuwa kitovu cha mjadala wa viongozi wa Umoja wa Ulaya.

Rais wa Baraza Kuu la Umoja huo, Charles Michel, alisema lengo la mkutano huo ni kuweka mazingira ya kufanya mazungumzo na Uturuki ili kuleta uthabiti na kuhakikisha uhuru na haki za mataifa wanachama wa Umoja wa Ulaya vinaheshimiwa.

Mahusiano kati ya Umoja wa Ulaya na Uturuki yamepwaya tangu serikali mjini Ankara ilipotuma meli ya utafiti mwezi Julai katika eneo la bahari linalozozaniwa.

**DW**

## Trump alitaka kundi la mrengo wa kulia kutulia

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amesema kundi la mrengo wa kulia linastahili kutulia na kuacha sheria kufanyakazi baada ya kukataa kulishutumu moja kwa moja katika mdahalo wa wagombea urais ulioendeshwa kupitia televisheni na kusababisha gumzo.

Katika mdahalo hulo, Trump alisema kuwa, "Sijui Proud Boys ni kina nani".

Siku moja baada ya kusema maneno hayo kwenye mdahalo na mpinzani wake, Joe Biden anataka kundi hilo kukaa kando na kuwa tayari.

Wanachama wa kundi la Proud Boys walisema matamshi yake ni kihistoria na ameliidhinisha.

Biden alisema Trump alikuwa amekataa kukana kundi la wazungu.

Mabadilishano hayo yalitokea wakati wa mjadala wa kwanza wa mahojiano ya kwenye televisheni kati ya wawili hao kabla ya uchaguzi unaotarajia kufanyika mwezi ujao.

**BBC**

HABARI MICHEZO




# ZIDANE
## HAJUI MAJALIWA YA HAZARD

**MADRID, Hispania**

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, hana uhakika Eden Hazard atakaa nje ya dimba kwa kipindi gani.

Hazard mwenye umri wa miaka 29, amekuwa na wakati mgumu pale Madrid na bado hajacheza mchezo wowote msimu huu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji alikuwa tayari kurudi dimbani baada ya kuumia kifundo cha mguu, lakini alipatwa na maumivu ya nyama za paja na kumfanya kuukosa mchezo wa Jumatano wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, wakati wakiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Real Valladolid.

Zidane hana uhakika na muda gani Hazard atakuwa nje ya dimba kabla ya kurudi dimbani.

"Siwezi kuwaambia kwa muda gani atakuwa nje ya dimba. Aliumia wakati akifanya mazoezi," alisema akiwaambia waandishi wa habari kuhusu maendeleo ya Hazard ambaye alitua hapo Real Madrid kwa uhamisho wa pauni milioni 100 kutoka Chelsea mwaka jana.

"Aliumia nyama za paja na amefanyiwa vipimo vinaonyesha kwamba ameumia na anatakiwa kuwa nje ya dimba.

"Amekuwa nje ya dimba kwa muda mrefu. Sifikirii kama na hii itamfanya kukaa kwa muda mwingi zaidi."

Hazard amekuwa na wakati mgumu tangu atue Madrid, ambako amefunga bao moja na kutoa pasi za mwisho tatu katika mechi 16 za LaLiga.

# Aouar mikononi mwa klabu tatu

**LYON, Ufaransa**

RAIS wa Lyon, Jean-Michel Aulas, amedai klabu kubwa tatu zinawania kumsajili kiungo wake, Houssem Aouar.

Arsenal imeonyesha nia ya wazi ya kutaka kumsajili Aouar kutoka Lyon, ingawa klabu hiyo ya Ligi Kuu England bado haijafikia ada inayotakiwa na miamba hao wa Ligue 1 ya pauni milioni 55.

Gazeti la Telefoot liliripoti Ijumaa iliyopita kwamba, Aouar amefikia makubaliano binafsi na Arsenal, ambao wameripotiwa wako tayari kutoa kiasi cha pauni milioni 36 kwa ajili ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22.



Hata hivyo, Aouar pia amekuwa akihusishwa na timu kama Manchester City, Chelsea na Paris Saint-Germain baada ya Lyon kuwa na msimu wa kuvutia wa 2019-20 walipotinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Mambo hayajafikiwa. Tunajua klabu tatu ambazo zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili Houssem," alisema Aulas akiwaambia waandishi wa habari Jumatano wakati alipoulizwa kuhusu hatima ya Aouar baada ya kuwasili kwa Lucas Paqueta kutoka Milan.

"Kuna baadhi ya klabu kubwa. Zote zimekuwa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na zilifanya vizuri. Mazungumzo ni magumu. Klabu haziko tayari kutoa kile tunachokitaka sisi."

Lyon imekuwa na mwanzo mgumu wa Ligi Kuu ya Ufaransa msimu huu wa 2020-21 kwani imeshinda mchezo mmoja tu kati ya mitano.

# Ancelotti ampigia debe Calvert - Lewin England

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti amemsifia Dominic Calvert-Lewin baada ya mshambuliaji huyo kufunga 'hat-trick' ya pili katika mechi nne.

Calvert-Lewin amefunga mabao nane katika mechi tano na juzi, Jumatano alifunga mabao matatu wakati Everton ikiibuka na ushindi wa 4-1 kwenye Kombe la EFL hatua ya 16 dhdi ya West Ham pale katika dimba la Goodison Park.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, alianza kufunga bao dakika ya 11 na akaongeza mawili baada ya Richarlison kufunga moja.

**Ancelotti amebainisha kwamba, Calvert-Lewin anastahili kuitwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya England wakati kocha, Gareth Southgate jana Alhamisi alitarajiwa kukitaja kikosi hicho.**

"Anafanya kazi nzuri kwa wakati huu. Kwa uhakika yupo kwenye kiwango cha kuvutia kabisa," alisema Ancelotti kuhusu Calvert-Lewin, ambaye alifunga hat-trick dhidi ya West Brom kwenye Ligi Kuu siku 11 zilizopita.

"Yupo kwenye kiwango bora sana kwa sasa. Naamini ni wakati sasa wa kuitwa timu ya Taifa ya England."



# ARSENAL

## YAIGOMEA ROMA KWA LACAZETTE

**LONDON, England**

ARSENAL imekataa ofa kutoka kwa klabu ya AS Roma ya kutaka kumsajili mshambuliaji wake, Alexandre Lacazette.

Miamba hiyo ya Emirates bado inataka kuboresha kikosi chao dirisha hili kabla halijafungwa, wakifukuzia huduma ya viungo wa Lyon, Houssem Aouar na Thomas Partey wa Atletico Madrid.

Hata hivyo, Arsenal inatafuta fedha za kunasa huduma za wachezaji hao na inatakiwa kuuza kwanza.

Kwa mujibu wa The Athletic, Roma wanahitaji sana saini ya Lacazette, lakini fedha waliyoweka mezani haijaishawishi Arsenal kumwachia mchezaji huyo raia wa Ufaransa.

Lacazette bado hajaanza mazungumzo yoyote kuhusu mkataba mpya na jambo hilo linawapa wasiwasi huenda anataka kuondoka. Mkataba wake wa sasa utafika tamati Juni 2022.



# PSG YAMWANIA DELE ALLI

**PARIS, Ufaransa**

PARIS Saint-Germain ipo tayari kumsajili Dele Alli ambaye kwa sasa anakabiliwa na wakati mgumu pale Tottenham Hotspur.

Dele hana uhusiano mzuri na kocha wake, Jose Mourinho hapo kwenye kikosi cha Spurs na PSG wanataka kumsajili raia huyo wa Uingereza kwa mkopo kabla ya dirisha hili la uhamisho kufungwa.

Mabingwa hao wa Ufaransa wamedai kwamba, watafikiria kumsajili jumla staa huyo, ili kumwondoa kwenye tatizo la Mourinho jumla.

Dele anaonekana kuwa tayari kuondoka baada ya kuwekwa benchi tu kwenye mechi mbili za ligi zilizopita.

Ripoti zinadai kwamba Mwenyekiti wa Spurs, Daniel Levy anafikiria kukubaliana na dili hilo.

Timu hizo zimekuwa na uhusiano mzuri, ambapo PSG iliwauzia Spurs wachezaji wawili, Lucas Moura na Serge Aurier katika miaka ya karibuni.

Alipoulizwa kuhusu Dele kukaa benchi, Mourinho alisema: "Kuna wengine pia wanasubiri kucheza. Haya ni mapambano ya ndani, mapambano baina ya marafiki. Kila mtu atapata nafasi ya kucheza."

Na alipoulizwa kama Dele atabaki Spurs hata baada ya dirisha kufungwa, Mourinho alisema: "Naamini hivyo."

# Wakala wa De Beek aijia juu Man United

**MANCHESTER, England**

WAKALA wa Donny van de Beek ameonyesha kutofurahishwa na namma hali ilivyo kwa mchezaji huyo pale Manchester United, kwani hajaanza katika mchezo wowote wa Ligi Kuu tangu aliponunuliwa kutoka Ajax.

Wakala, Sjaak Swart ameuambia mtandao wa VoetbalPrimeur kwamba, hapendi kuona mteja wake huyo akitokea benchi.

"Hata mimi binafsi siwezi kulifanya, anasimamishwa zikiwa zimebaki dakika nne," alisema Swart.

Kiungo huyo wa kimataifa wa Uholanzi alijiunga na Man United kwa uhamisho wa pauni milioni 40, mashabiki wamekuwa wakitamani kumwona akicheza sambamba na Bruno Fernandes na Paul Pogba.

Hata hivyo, alionekana akiingia katika mechi zao mbili za ligi, akicheza kwa dakika 23 dhidi ya Crystal Palace na akiingia pia dakika za mwisho katika mchezo dhidi ya Brighton.

Mchango wake ulikuwa mkubwa katika michezo yote, alifunga katika mchezo dhidi ya Palace na pia alisababisha penalti katika mchezo dhidi ya Brighton, wakati Man United ililazimishwa sare.

"Alifanya vitu vitatu zaidi vizuri," alisema Swart. "Penalti, ambayo walipata bao la tatu, lilitokea kwake. Wangeweza kufungwa hata mabao 7-1. Brighton waligongesha nguzo mara tano. Wana timu nzuri, lakini halitakiwi kutokea kwa Manchester United."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER: SISHANGAZWI NA KIWANGO CHA MATA

Ni mchezaji mtulivu akiwa na mpira na anajua nini anachokifanya uwanjani, hivyo kiwango chake kwangu mimi si cha...

**MANCHESTER, England**

OLE Gunnar Solskjaer "kamwe hajawahi kushangaa" kuona Juan Mata akitawala mchezo baada ya kiungo huyo kufunga bao moja na kutengeneza jingine, wakati Manchester United ikiibuka na ushindi wa 3-0, dhidi ya Brighton and Hove Albion kwenye mchezo wa EFL, juzi Jumatano.

Mata alimtengenezea pande Scott McTominay aliyefunga bao la kwanza kwa United kwenye mchezo huo wa Jumatano wa hatua ya 16, kabla ya kutumia vizuri pasi ya Donny van de Beek na kufunga bao lake la 50, kwa klabu hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, pia alifunga katika hatua ya tatu katika ushindi dhidi ya Luton Town na amehusika katika mabao 13 katika mechi 15, zilizopita ambazo alianza kwa United.

Mata hakuwa sehemu ya kikosi cha Solskjaer katika mechi mbili za ufunguzi za Ligi Kuu, lakini kocha huyo mkuu wa United ana furaha kuona mchango wa Mhispania huyo.

"Kilikuwa kiwango cha kuvutia kwa Juan Mata," Solskjaer alisema akiiambia Sky Sports. "Alikuwa akipata mpira anatulia.

"Ni mtu ambaye anajua nini anachokifanya na alitengeneza bao safi kabisa. Nishawahi kushangazwa kwa kiwango chake.

"Ni mchezaji mtulivu akiwa na mpira na anajua nini anachokifanya uwanjani, hivyo kiwango chake kwangu mimi si cha kushangaza."

Ushindi huo wa United ulikuwa ni wa tatu mfululizo kwenye mashindano yote, siku nne baada ya kutoka kushinda 3-2, dhidi ya Brighton katika uwanja huo huo kwenye mchezo wa Ligi Kuu.

Paul Pogba alifunga bao la tatu zikiwa ni dakika 11 tu baada ya kuingia dimbani akitokea benchi.

## KWA UFUPI

**ARSENAL PAZURI KWA AOUAR**
Arsenal wameongeza jitihada za kumshawishi kiungo wa kati anayekipiga Lyon, Houssem Aouar mwenye umri wa miaka 22, huku Rais wa klabu hiyo, Jean- Michel Aulas, akikiri kuwa wanaweza "kuwapoteza wachezaji wawili" kabla ya kufungwa kwa pazia la usajili. ***(Metro)***

**UNITED YAJITOSA KWA DEMBELE**
MANCHESTER United imeanza mazungumzo na Barcelona kuhusu kumnyakua kwa mkopo mshambuliaji Mfaransa, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 23. ***(Mirror)***

**COUTINHO KUINUFAISHA LIVER**
LIVERPOOL pia wamejiandaa kufaidika na kiungo wao wa zamani, Philippe Coutinho wa Barcelona kwa kupata kitita cha pauni milioni 4.4, ikiwa raia huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 28, atacheza mechi nyingine 14. ***(Mirror)***

**SPURS YAMSAJLI VINICIUS**
KLABU ya Tottenham Hotspur wamemaliza makubaliano ya kumsajili kwa mkopo mshambuliaji wa Benfica, Carlos Vinicius mwenye umri wa miaka 25, ambaye gharama ya kumsajili moja kwa moja ni pauni milioni 89, kwa mujibu wa kifungu cha mkataba wake. ***(Mail)***

**JOVIC AWANIWA UNITED**
WAKALI wa mshambuliaji wa Real Madrid, Luka Jovic mwenye umri wa miaka 22, amesema raia huyo wa Serbia anataka kujiunga na Manchester United, huku inter Milan na Roma zikimtolea macho pia. **(Star)**

**LIVER KUMUUZA BREWSTER**
LIVERPOOL wanajiandaa kukubali ofa ya pauni milioni 23 kutoka Sheffield kwa ajili ya mshambuliaji, Rhian Brewster. ***(Sun)***

**UTD WAKANA KUHUSISHWA MAITLAND-NILES**
KLABU ya Manchester United wamekataa kuhusishwa kwao na taarifa za kumsajili Ainsley Maitland-Niles mwenye umri wa miaka 23, ambaye anaweza kucheza nafasi ya ulinzi na kiungo wa kati, kutoka Arsenal. ***(Manchester Evening News)***

**CHELSEA KUUZA WATATU**
CHELSEA inaweza kuongeza wachezaji wa kuondoka kwenye klabu hiyo kwa kumuuza mlinzi Marcos Alsonso mwenye umri wa miaka 29, beki wa kati Antonio Rudiger mwenye miaka 27 na kiungo wa kati Ruben Loftus-Cheek, 24, kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili. ***(Star)***

**NEWCASTLE YAMFUATA RUGANI**
KLABU ya Newcastle United inajiandaa kupambana na Valencia katika mbio za kuwania kumsajili mlinzi wa Juventus, Daniele Rugani, ambaye pia anahusishwa na taarifa za kutakiwa na Fulham, West Ham na Sevilla. ***(Sportitalia)***

**ARSENAL KUMTOA GUENDOUZI**
KLABU ya Arsenal ipo kwenye mazungumzo ya kumtoa kwa mkopo kiungo wao wa kati, Matteo Guendouzi kwenda Marseille. ***(Telefoot via Express)***

**ASTON VILLA KUMSAJILI SMITH**
KLABU ya Aston villa ipo mbioni kumsajili beki wa kati, Kerr Smith mwenye umri wa 15, kutoka Dundee United. ***(Dundee Telegraph)***

**WALCOTT BADO YUPO EVERTON**
KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti hatarajii winga Theo Walcott mwenye umri wamiaka 31, ataondoka katika klabu hiyo kipindi hiki cha usajili. ***(Mail)***

**PEREIRA AWANIWA LAZIO**
LAZIO ipo katika mazungumzo ya kumsajili kiungo wa kati wa Manchester United raia wa Brazil, Andreas Pereira mwenye umri wa miaka 24, kwa mkopo wa muda mrefu. ***(Telegraph)***

## HABARI MICHEZO

# KAGERE, BOCCO, MUGALU WAMPA MTIHANI SVEN

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imeweka wazi kufurahishwa na uwapo wa washambuliaji watatu mahiri, Meddie Kagere, John Bocco na Chris Mugalu kuwa unainufaisha na kuchochea kufanya vizuri kwa timu kwa sababu kila mmoja anataka aanze kwenye kikosi cha kwanza.

Mkuu wa Idara wa Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Haji Manara amesema tofauti na watu wanavyofikiria kuwa wachezaji hao hawana furaha, bali hali hiyo ya kuwa na washambuliaji watatu, huku Kocha Sven Vandenbroeck akipenda kumuazisha straika mmoja tu, kumeleta hali ya kupambana kuwania namba kwao.

"Hata mazoezini unaona kabisa, kila mmoja anapambana, watu wanagongana kusaka namba, na kila mtu anapopewa nafasi anataka aonyeshe kuwa yeye ndiye anapaswa aanze, iwe alianza mwanzo, au aliingia kipindi cha pili," alisema Manara kwenye mazungumzo maalum na Nipashe wakati wa ziara yake katika ofisi za gazeti hili.

Alisema ni kweli kabisa kocha wao si muumini wa kuchezesha washambuliaji wawili, hivyo kutokana na hali hiyo, ni lazima mmoja acheze, mwingine awe benchi na wengine wawili wawe jukwaani.

"Kwa hali hiyo kila mmoja sasa anapambana ili amshawishi kocha kuanza kwenye mechi, ndiyo maana unaona kuna wakati Bocco alikuwa akianza, na sasa Kagere anaanza na Mugalu anaingia, Bocco amekaa jukwaani," alisema.

Hivi karibuni kocha Sven alisema kuwa anachezesha mshambuliaji mmoja kwa sababu si lazima magoli yafungwe na washambuliaji, badala yake anatengeneza mfumo wa kila mmoja anayepata nafasi aitumie.

Kwa muda mrefu sasa baadhi ya wanachama na mashabiki wa Simba wameonekana kupingana na kocha wao kutokana na mfumo huo anaoupenda wa kutumia mshambuliaji mmoja mbele, tofauti na kocha aliyeondoka Patrick Aussems ambaye alikuwa akipenda kutumia washambuliaji wawili mpaka watatu wakati mwingine.

Aussems alipenda kuwatumia Bocco, Kagere na Emmanuel Okwi kwa wakati mmoja na kuifanya Simba kushambulia muda wote wa mchezo, ingawa wakosoaji wanadai kuwa mfumo huo ndiyo uliokuwa ukisababisha timu hiyo kufungwa idadi kubwa ya mabao inapokwenda kucheza ugenini, hasa kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Mpaka sasa Kagere na Mugalu wana magoli mawili kila mmoja, ingawa mara nyingi hawaanzi kwenye kikosi hicho.

Kwenye mechi nne za Ligi Kuu ambazo Simba imecheza, Kagere alianza kwenye mechi mbili dhidi ya Biashara, Simba ikishinda mabao 4-0 na kisha ikaichapa Gwambina 3-0 na katika mechi hizo, Mugalu akiingia akitokea benchi alifunga zote mbili.

Kwa upande wa Bocco ambaye alianza kwenye mechi mbili za mwanzo, dhidi ya Ihefu FC na Mtibwa Sugar, amefunga bao moja kwenye mechi ya ufunguzi dhidi ya Ihefu Simba ikishinda mabao 2-1.

# Mtibwa yatoa wiki mbili kurudi Jamhuri

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Mtibwa Sugar, umesema ndani ya siku mbili wataweka wazi uwanja watakaoutumia baada Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kufungia Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro waliokuwa wakiutumia kama wa nyumbani, lakini pia ukieleza kuwa wanauhakika marekebisho waliyoelekezwa kuyafanya yatakamilika haraka iwezekanavyo.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mkurugezi wa timu hiyo, Jamal Bayser,alisema baada ya kufungiwa uwanja wao huo wapo katika mchakato wa kumulika uwanja mwingine na ndani ya siku mbili watautangaza.

Alisema licha ya kupangwa kutumia Uwanja wa CCM Gairo uliopo mjini humo, pia wanaangalia uwanja mwingine ambao utakuwa na vigezo vya kucheza mechi zao za ligi hadi hapo ule wa Jamhuri utakapokamilika.

"Baada ya kupata taarifa kutoka Bodi ya Ligi kuwa uwanja wetu umefungiwa tulianza marekebisho ambayo mpaka sasa yanaendelea vizuri, tunaamini Mungu akipenda mpaka baada ya wiki mbili kuenda ukawa umekamilika na kuruhusiwa kuendelea kuutumia kama kawaida,"alisema Bayser.

Alisema mashabiki waondoe presha kuhusu suala hilo la uwanja, wakitarajia baada ya wiki mbili, Jamhuri utakuwa umefanyiwa maboresho na kuruhusiwa kurejea kuutumia kama uwanja wao wa nyumbani mara baada ya kurudi kutoka Kanda ya Ziwa.

Bayser alisema mechi yao ijayo, itakuwa Jumapili dhidi ya Biashara United ugenini, pia akiweka wazi mikakati yao msimu huu kuwa wamejipanga kushika nafasi za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu baada ya kutofanya vizuri msimu uliopita, licha ya kwamba walitwaa ubingwa wa Kombe la Mapinduzi baada ya kuifunga Simba katika mechi ya fainali.

Alisema moja ya mikakati hiyo walianza kwa kufanya usajili mzuri wa wachezaji kwa kuziba nafasi zote ambazo zilionekana kuwa na upungufu hadi kuwasababishia kunusurika kushuka daraja.

"Tutahakikisha msimu huu tunafanya vizuri ikiwa ni pamoja na kushika nafasi za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu, tunaomba mashabiki na wapenzi wetu wasivunjike moyo bali waendelee kutupa ushirikiano ili tutimize mipango tuliyojiwekea,"alisema.

**PAMOJA SANA...**



Mshambuliaji wa kimataifa wa Tanzania, Thomas Ulimwengu (kulia), akifurahi na wachezaji wenzake wa TP Mazembe baada ya mazoezi ya timu hiyo juzi mjini Lubumbashi, DR Congo. **PICHA: MTANDAO**

## JKT kuzoa mamilioni wakiichapa Simba

**Na Saada Akida**

WACHEZAJI wa JKT Tanzania, wameahidiwa mamilioni ya shilingi endapo watafanikiwa kubakiza pointi tatu katika mechi yao ijayo dhidi ya Simba itakayopigwa Jumapili katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Katibu Mkuu wa timu hiyo, Abdul Nyumba, alisema wamekuwa na desturi ya kutoa hamasa kwa wachezaji wao wanaposhinda ila mechi dhidi ya Simba kuna baadhi ya wadau ndani ya taasisi hiyo wameahidi kuongeza fedha endapo pointi tatu zitapatikana.

Licha ya kutokuwa tayari kutaja kitita hicho kitakuwa milioni ngapi, alisema wachezaji wao wanatambua umuhimu wa kila mechi, ila ahadi hizo za fedha ni kwa ajili tu ya kuwapa hamasa na motisha ili kupambana zaidi kuhakikisha wanapata matokeo mazuri ya ushindi.

"Hii ni mechi nzuri sana, ukizingatia tunacheza na mabingwa mbali na ahadi yetu ya kawaida, lakini pia kuna baadhi ya viongozi ambao wapo ndani ya taasisi hii wameahidi kuongeza fedha endapo tutafanikiwa kumfunga Simba," alisema Nyumba.

Kwa mujibu wa benchi la ufundi linaloongozwa na kocha Abdallah Mohammed, kikosi chao kinaendelea vizuri na mazoezi kwa ajili ya kukabiliana na Simba katika mchezo huo.

## Simbu aanza rasmi maandalizi Olimpiki

**Na Shufaa Lyimo**

MWANARIADHA wa mbio ndefu, Alphonce Simbu, anaendelea na mazoezi ya kujiandaa na mashindano ya Olimpiki yatakayofanyika mapema Julai mwakani nchini Japan.

Akizungumza na gazeti hili jana, kocha wa mchezaji huyo, Anthony Muingereza, alisema kwa sasa anampa mazoezi ya kukimbia kilometa 25 -30 kwa asubuhi, na jioni anakimbia kilometa 10-15 kwa lengo la kumuimarisha na kuwa sawa kuelekea katika mashindano hayo makubwa yatakayoshirikisha nchi mbalimbali.

"Tupo kwenye mchakato wa kumtafutia Simbu mashindano ya majaribio nje ya nchi, ikiwamo kukimbia mbio ndefu kwa ajili ya kuhakikisha anakuwa na pumzi zaidi ili mashindano yatakapoanza awe vizuri na kufanikiwa kutwaa medali,"alisema Muingereza.


Alisema hapo awali alishindwa kumpa mwanariadha wake mazoezi kutokana na janga la virusi vya corona, lakini kwa sasa anampa muda mfupi wa kupumzika kuliko wa kufanya mazoezi.

Pia ametoa wito kwa wanariadha wote ambao wamefuzu kwenda kushiriki mashindano hayo ya Olimpiki kujitahidi kufanya mazoezi.

Kwa upande wa Simbu, alisema anaendelea vizuri na program ya mazoezi anayopewa na mwalimu wake huyo ambayo hufanya mara mbili kwa siku ikiwamo kukimbia pembeni mwa Mlima Meru jijini Arusha.

"Mbali na kukimbia pembeni ya Mlima huo, pia nakimbia barabarani kwa sababu nakwenda kushiriki mashindano makubwa ya dunia, lengo langu ni kuhakikisha naenda kuipeperusha vema bendera ya Tanzania," alisema Simbu.

Michezo
Ijumaa Oktoba 2, 2020
Nipashe



SOLSKJAER: SISHANGAZWI NA KIWANGO CHA MATA HABARI UK 22

## YANGA HESABU KWA COASTAL UNION KESHO

**Na Saada Akida**

HUKU kikosi cha Yanga kikizidi kulalamikiwa na mashabiki wake kwa kushindwa kuonyesha soka la kuvutia, huku kila mchezaji akibaki kucheza kwa uwezo wake binafsi uwanjani, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Juma Mwambusi amesema mechi za kirafiki wanazocheza zinawasaidia kupata mwanga wa aina ya wachezaji ambao wanaweza kuwasaidia katika Ligi Kuu pamoja na kupata muunganiko kikosini.

Yanga juzi usiku iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya KMKM ya Zanzibar katika mechi ya kirafiki iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam, ikiwa ni maandalizi ya kuikabili Coastal Union kesho katika Uwanja wa Mkapa.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mwambusi alisema wachezaji wao ni wazuri na wanauwezo mkubwa, lakini wanahitaji kupata wachezaji ambao wanaweza kupambana kulingana na mpinzani wao wanayetarajia kukutana naye katika ligi hiyo.

Alisema mbali na kupata mwanga huo, lakini wanatengeneza ushindani mkubwa wa wachezaji wao kuhakikisha wanapata namba katika kikosi cha kwanza na kusaidia kupata matokeo chanya kwa kila mechi.

"Mechi hizi zinawasaidia kujiandaa na mchezo unaofuata wa ligi, lakini kutupa mwanga benchi la ufundi, kuona mchezaji gani atatusaidia katika mechi ipi, kuna jambo ambalo tunaliona ndani ya kikosi tunachokijenga ikiwamo kujenga ushindani zaidi kwa wachezaji wetu," alisema Mwambusi.

Kuhusu mechi dhidi ya Coastal Union, Mwambusi alisema wanaimarisha kikosi chao kuhakikisha wanaendeleza moto wao wa kupata matokeo mazuri kwa kuvuna pointi tatu katika mechi hiyo.

Kwa upande wa kiungo wa timu hiyo, Haruna Niyonzima, alisema wamejiandaa vizuri kwa ajili ya mechi yao dhidi ya Coastal kwa kuhakikisha wanapambana kutafuta pointi tatu muhimu.

"Sio kazi nyepesi kupata ushindi ndani ya uwanja ila inahitaji maandalizi mazuri, tunachokifanya kwa sasa ni kuona tunakuwa na timu bora itakayotupa matokeo, tutapambana mbele ya Coastal Union kupata ushindi," alisema Niyonzima.

KAPOTEA...



Raheem Sterling akimpoteza kipa wa Burnley, Bailey Peacock-Farrell, na kuifungia Manchester City bao la pili dakika ya 49 ikiwa ni dakika 14 baada ya kufunga la kwanza wakati wakishinda 3-0 kwenye mchezo wa 16-Bora wa Kombe la Ligi England (Carabao Cup) na kutinga robo fainali. Bao la tatu lilifungwa na Ferran Torres dakika ya 65. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YAFUATA TATU ZA JKT NA UBINGWA

## Kulala na mashabiki Morogoro leo wakisherehekea kabla ya Jumamosi kutua Dodoma, Sven asema...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba, leo wakianza safari ya kuifuata JKT Tanzania katika mechi yao ya raundi ya tano itakayopigwa katika Uwanja wa Jamburi jijini Dodoma Jumapili wiki hii, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Sven Vandenbroeck, amesema kutokana na kikosi chake kuzidi kuimarika ana matumaini makubwa ya kupata matokeo chanya katika mechi zake zinazofuata.

Simba itaondoka kwa basi leo ambapo italala mkoani Morogoro kwa ajili ya kusherehekea kombe la ubingwa na mashabiki wao kisha kesho alfajiri kuanza safari ya kuelekea Dodoma ikiwa na taji hilo la ubingwa walilolitwaa msimu uliopita kwa mara ya tatu mfululizo.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Haji Manara, alisema jana kuwa baada ya timu kuwasili jijini Dodoma Jumamosi itafanya mazoezi jioni kwenye Uwanja wa Jamhuri kujiweka sawa kabla ya mchezo huo wa Jumapili.

Manara alisema wachezaji wote wapo kwenye hali nzuri, huku nahodha John Bocco afya yake ikiimarika na kama kocha Sven ataona inafaa anaweza kumtumia katika mechi hiyo.

"Kikosi kitaondoka kesho (leo) kuelekea Dodoma, lakini tutapitia Morogoro kwa ajili ya kusherehekea pamoja na mashabiki wetu tukiwa na kombe letu la ubingwa na siku itakayofuata tutaelekea makao makuu ya nchi kwa ajili ya mechi dhidi ya JKT," alisema Manara huku akieleza kuwa hadi sasa kiungo Mbrazil Gerson Fraga, ndiye pekee atakayekosa mchezo huo kutokana na kuendelea kuuguza jeraha lake.

Kwa upande wa Kocha Mkuu, Sven, alisema wachezaji wake wanazidi kuimarika kila siku, jambo linalompa matumaini ya kuondoka na pointi tatu katika mechi zao zijazo.

Simba itaivaa JKT Tanzania ikiwa na kumbukumbu ya kupoteza mechi yake ya raundi ya pili kwa kipigo cha bao 1-0 dhidi ya timu hiyo msimu uliopita, lakini ikiwa ni baada ya 'Wekundu wa Msimbazi' hao kushinda 3-1 katika mzunguko wa kwanza.

"Kwa ujumla wachezaji wangu wanazidi kuimarika kuwa bora, kila baada ya mechi tunafanyia kazi kasoro zinazojitokeza ili kuona namna gani wataweza kuwa bora zaidi.

"Bado tatizo linabaki kwenye safu ya ushambuliaji kushindwa kutumia vema nafasi tunazo tengeneza, hilo ni suala ambalo tunaendelea kulifanyia kazi," alisema kocha huyo raia wa Ubelgiji.

Simba yenye pointi 10 ikiwa nafasi ya pili nyuma ya vinara Azam FC wenye alama 12, itashuka dimbani ikitaka kuendeleza ushindi wao wa mabao 3-0 waliopata dhidi ya Gwambina FC katika mechi iliyopita, lakini JKT Tanzania ambayo hadi sasa imejikusanyia alama nne ikiwa na nafasi ya 13 kwenye msimamo wa ligi hiyo, yenyewe imetoka kupoteza kwa kufungwa bao 1-0 ugenini dhidi ya Coastal Union.

Baada ya mechi hiyo, ligi hiyo itasimama kupisha Kalenda ya Fifa, na mechi itakayofuta, Simba watakuwa wageni wa Yanga kwenye mechi ya 'dabi' itakayopigwa Uwanja wa Mkaba Oktoba 18, mwaka huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >